

10 SIKU ZA MAOMBI

YALIYOMO:

Vipaumbele vya Imani – Mwongozo wa Kiongozi	2
Utangulizi	10
Usiku wa Maombi	18
Changamoto za Kuwafikia watu walio nje	20
Ahadi za Kudai kwenye Maombi	23
Sherehe ya Siku ya Sabato	33
Mahitaji ya Kucombea ya Kanisa la Kiulimwengu.....	35
Siku ya 1 – Wingi si Hoja	41
Siku ya 2 – Hatari ya Kukosa Nafasi kwa Mungu	45
Siku ya 3 – Baraka ya Kusubiri	49
Siku ya 4 – Uhuru wa Kuchagua Maisha Rahisi	52
Siku ya 5 – Kujali Mambo Muhimu Katika Maombi Yetu	56
Siku ya 6 – Ujasiri, Shauku Kali na Uvumilivu	60
Siku ya 7 – Thamani ya Kuwa Mwema	64
Siku ya 8 – Kuwa na Shukrani	67
Siku ya 9 – Mbaraka wa Sabato	70
Siku ya 10 – Ujazwe na Vitu vya Muhimu	74

VIPAUMBELE VYA IMANI

MWONGOZO WA KIONGOZI

Karibu tena katika Siku Kumi za Maombi mwaka 2024! Tunaamini kuwa, katika maombi ndipo mahali uamsho unapozaliwa. Mungu ametenda miujiza mingi katika miaka iliyopita kadiri tulivyokuwa tukimtafuta katika maombi na kufunga. Roho Mtakatifu amewezesha uamsho, mabadiliko, hisia za uinjilisti zilizojengwa upya, makanisa yaliyoamshwa, na mahusiano yaliyoponywa.

Je, sauti ya Mungu imekuwa ikikuita kufanya uamsho?

Biblia imejaa ahadi kwa ajili yako:

“Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao” (2 Nyakati 7:14).

“Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote” (Yeremia 29:13).

“Na itakuwa ya kwamba mtu awaye yote atakayeliitia jina la Bwana ataponywa” (Yoeli 2:32).

“Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi” (Yakobo 4:8).

“Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na ye ye pamoja nami” (Ufunuo 3:20). Po pote ulipo katika maisha wakati huu wa sasa, Mungu yupo karibu na wewe zaidi kuliko unavyofikiria. Anataka kumwaga mibaraka yake Yake kwa familia yako, kwa kanisa lako, kwa jamii yako, na kwa ulimwengu wako.

10 SIKU ZA MAOMBI

Mambo ya kawaida ya maombi katika siku kumi za maombi

Miongozo ya Maombi ya Kila Siku

Tumetoea mwongozo wa maombi ya kila siku katika siku hizi kumi. Mwongozo wa kila siku husika unajumuisha aya ya Biblia itakayotumika katika kuomba, somo la keshakwa ajili ya maombi, aya za Biblia za kutumia katika kuomba, mapendekezo ya maombi, na mapendekezo ya nyimbo. Tunashauri kuwa ikiwezekana utoe nakala ya kurasa za miongozo ya kila siku ili kila mshiriki aweze kuwa na nakala yake apate kufuatisha katika ule muda wa maombi. Makanisa ulimwenguni yataungana katika kuomba yakijikita katika mada ya siku husika. Ungana nao katika kuomba kupitia katika aya na mahitaji yaliyoletwa, lakini usihisi kwamba unapaswa kupitia kwa haraka katika orodha yote ya mahitaji ya maombi. Mnaweza kugawanyika katika vikundi vidogo na kila kikundi kikaombea sehemu ya orodha ya mahitaji yenu ya kuombea

Pia tumejumuisha ukurasa unaoitwa Maombi ya Kanisa la Kiulimwengu. Ni muhimu kuomba pamoja kwa ajili ya familia ya kanisa letu la kiulimwengu, lakini unaweza kutenga muda zaidi wa kuombea mahitaji ya sehemu mahalia ikiwa kundi lako linajumuisha wageni kutoka katika jamii husika. Ombo kuhusu namna unavyoweza kuwakaribisha wageni kwa ubora zaidi na kuwafanya wajisikie kuwa ni sehemu ya kundi hilo.

Muda unaopendekezwa kwa ajili ya kila Kipengele cha Maombi

Fanya muda wenu wa maombi kuwa wa kawaida na rahisi kadiri iwezekanavyo ili kikundi chenu kiweze kuelekeza mawazo katika kuomba. Muda utakaotumika katika kila kipengele utatofautiana. Mwongozo ufuatao ni mapendekezo tu:

- Kukaribisha/UtanguliziUkaribisho na utangulizi – dakika 2 hadi 5

10 SIKU ZA MAOMBI

- Usomaji wa "Kesha" Soma somo la maombi (mwongozo wa maombi wa kila siku) - dakika 5
- Kuomba Kupitia mafungu katika "Kuomba kwa Neno la Mungu" (mwongozo wa maombi wa kila siku) - dakika 10 hadi 15
- Kuombea mahitaji katika "Mapendeleko zaidi ya Maombi" (mwongozo wa maombi wa kila siku) - dakika 20 hadi 30
- Kushukuru kwa nyimbo na sifa - dakika 5 - 10

Kuombea Wengine

Hamasisha kila mtu kuombea watu watano hadi saba ambao Mungu ameweka katika maisha yao. Wanaweza kuwa ndugu, marafiki, wafanyakazi wenza, majirani, au watu wanaofahamiana nao. Wahamasishe kumwomba Roho Mtakatifu awaongoze katika kuchagua majina ya watu hao na kuhakikisha wanawafikia ndani ya siku hizi kumi za maombi. Unaweza kutoa kadi au vikaratasi ambavyo watu watatumia kuandika majina watakayokuwa wakiombea.

Huduma za Sabato katika Kipindi cha Siku Kumi za Maombi

Maombi na yalenge katika kitu mahususi, na ni vyema kushiriki pamoja shuhuda mbali mbali za maombi yaliyojibiwa katika huduma siku ya Sabato kanisani Jumamosi zote mbili. Iweni wabunifu - kuna namna nyingi za kushiriki pamoja na familia ya kanisa mambo yanayotokea katika mikutano ya maombi ya kila siku.

Sherehe ya Sabato ya Kuhitimisha

Sabato ya mwisho inapaswa kutayarishwa kwa namna itakayokuwa ni muda wa furaha kuu kwa yale yote Mungu aliyotenda katika siku hizi kumi. Tenga muda wa kutosha kwa ajili ya shuhuda za maombi yaliyojibiwa, kwa ajili ya mafundisho ya kibiblia/mahubiri juu ya maombi, na kwa

10 SIKU ZA MAOMBI

ajili ya nyimbo. Ongoza kusanyiko katika muda wa maombi ili kwamba hata wale ambao hawakuhudhuria mikutano ya kila siku, wapate uzoefu wa furaha ya kuomba pamoja na wengine. Tafadhali tazama mwongozo wa Sherehe za Sabato kwa mawazo zaidi.

Kufuatilia kipindi hiki cha maombi ya siku kumi

Omiba ili kupata ufahamu jinsi Mungu anavyotaka kanisa au kikundi chako kuendeleza kile Alichanzisha katika kipindi hiki cha Siku Kumi za Maombi. Pengine mtaendelea kukutana kila juma kwa ajili ya maombi. Au pengine Mungu anataka muanze huduma mpya ndani ya kanisa lenu au katika kuifikia jamii. Muwe tayari na kumfuata Mungu kule anapowaelekeza. Hakika mtashangazwa kadiri mnavyotembea pamoja naye. Ukurasa wa kwa ajili ya Changamoto ya Kuwafikia Wengine umejaa mawazo ya huduma.

Shuhuda

Tafadhali shiriki visa vinavyoonesha jinsi Mungu alivyotendakazi katika Siku Kumi za Maombi! Visa vyako vitakuwa msaada na hamasa kwa wengine wengi. Shuhuda zinaweza kutumwa mtandaoni kwenye tovuti hii: www.tendaysofprayer.org.

Vielekezi vyta Muunganiko katika Maombi

Kubalianeni

Mtu anapoombea hitaji fulani kwa Mungu, hakikisha kuwa wengine pia wanaombea hitaji hilo hilo na kukubaliana - kufanya hivi kuna nguvu! Usifikiri kwamba kwa sababu mtu mmoja ameomba kuhusu hitaji hilo, hakuna haja ya mwingine kuliombea. "Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni" (Mathayo 18:19). Inatia moyo kiasi gani

10 SIKU ZA MAOMBI

kuinuliwa katika maombi!

Kudai Ahadi za Mungu

Hamasisha kikundi kudai ahadi za Mungu kadiri wanavyoomba. Ni rahisi sana kujielekeza katika matatizo yetu. Lakini tunapodai ahadi za Mungu, tunaongeza imani yetu na kujikumbusha kwamba hakuna kinachoshindikana kwa Mungu. Ahadi hizo hutusaidia kuondoa macho yetu kwenye madhaifu yetu, na magumu tunayokabiliana nayo, hivyo kuyaelekeza kwa Yesu. Tunaweza kupata ahadi za Biblia za kudai kwa kila udhaifu na kila pambano. Himiza watu kutafuta ahadi nyangi zaidi kadiri iwezekanavyo na kuziandika ili waweze kuzidai katika maombi wakati ujao.

Kufunga

Alika wale wanaoungana nawe katika Siku Kumi za Maombi kufikiria aina ya kufunga watakayoshiriki, kwa mfano kufunga na kuacha kutazama televisheni, kuacha kusikiliza muziki wa kidunia, kuacha kutazama filamu, kuacha kuingia mtandaoni, kuacha kula vitu vitamu vitamu kama vile pipi, au aina nyiningine ya vyakula ambavyo ni vigumu kumeng'enywa. Tumia muda wa ziada katika kuombe na kujifunza Biblia, ukimwomba Mungu akusaidie wewe na kusanyiko lako kudumu kikamilifu zaidi katika Kristo. Kwa kuchagua mlo mwepesi, tunaruhusu akili zetu kuwa sikivu zaidi kwa sauti ya Roho Mtakatifu.

Roho Mtakatifu

Hakikisha unamwomba Roho Mtakatifu akuonyeshe jambo la kuombea katika maisha ya mtu fulani au katika hali fulani. Biblia inatuambia kwamba hatufahamu tuombe nini, na kwamba Roho Mtakatifu ndiye anayetuombea.

"Hatupaswi kuomba tu kwa jina la Kristo, bali kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Hii huelezea maana halisi tunaposema kuwa Roho "hutuombea kwa kuugua kusikoweza

10 SIKU ZA MAOMBI

kutamkwa." (Warumi 8:26). Mungu hufurahia kujibu ombi kama hilo. Tunapoomba kwa dhati na kwa nguvu tunaomba kwa jina la Kristo, katika nguvu hiyo kuna ahadi kutoka kwa Mungu kwamba anakaribia kujibu maombi yetu kama tunavyosoma kuwa, "Basi atukuzwe yeze auezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu" (Waefeso 3:20)" (Christ Object Lessons, uk. 147, msisitizo umeongezewa).

Kutunza Taarifa ya Maombi

Kutunza daftari la kumbukumbu ya maombi kwenye kipindi chote cha Siku Kumi za Maombi kunaweza kuwa njia bora ya washiriki kuhifadhi moyoni wazo kuu la maombi ya kila siku, kufanya maagano thabiti na Mungu, na kutambua mibaraka yake kwao. Kuorodhesha maombi yetu na kutunza kumbukumbu ya majibu ya Mungu ni njia iliyothibitishwa ya kutia moyo.

Ikiwa utapenda, unaweza kutenga muda pale mnapokutanika kwa ajili ya maombi, ili watu wapate kuandika mwitikio wao kwa Mungu kwenye shajara zao binafsi za maombi. Au unaweza kutunza shajara ya kikundi cha maombi na majibu yake – linaweza kuwa ni daftari, au bango kubwa, au unaweza kutunzia mtandaoni. Inafurahisha na pia inajenga imani unapotazama nyuma na kuona jinsi Mungu alivyojibu maombi!

Kicho

Himiza na kujenga mtazamo wa kicho na unyenyekevu. Tunakaribia chumba chenye kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu. Hebu tusitumie muda huu wa maombi vibaya kwa mkao na kwa mwenendo wetu usiofaa na hata katika mazungumzo yetu. Hata hivyo, siyo lazima kila mmoja apige magoti muda wote. Unahitaji watu wawe huru kwa saa moja, hivyo wahamasishe watu kupiga magoti au

10 SIKU ZA MAOMBI

kukaa au kusimama kadiri Mungu atakavyokuongoza na kwa namna wanavyokuwa huru zaidi.

Maombi Kuwa ya Sentensi

Maombi yanapaswa kuwa mafupi, na yaelekezwe moja kwa moja kwenye hitaji. Kufanya hivi kutawapatia wengine pia fursa ya kuomba. Jaribu kufupisha maombi yako yawe ni ya sentensi chache. Kila mmoja anaweza kuomba mara kadhaa. Maombi mafupi yatafanya kipindi cha maombi kiwe cha kufurahisha na siyo cha kuchosha na hivyo kumruhusu Roho Mtakatifu aguse kundi zima akiwaonesha namna ya kuomba. Siyo lazima kuanza na kumaliza ombi fupi la sentensi kwa maneno kama "Mungu wetu mpPENDWA" na "Amina." Ni mawasiliano endelevu na Mungu.

Ukimya

Wewe kama kiongozi, usitawale kipindi cha maombi. Lengo kubwa ni kuwawezesha wengine kuomba. Kipindi cha ukimya kina thamani kubwa ajabu, kwani humpa Mungu muda wa kuzungumza na mioyo yetu. Mruhusu Roho Mtakatifu afanye kazi kwa kumpa kila mmoja muda wa kutosha wa kuomba.

Kuimba

Nyimbo za hapa na pale kutoka kwa vikundi, zikiunganishwa kwenye maombi, huongeza uzuri katika mkutano wa maombi. Nyimbo zilizopendekewa zimeorodheshwa mwisho wa kila ukurasa wa wazo la siku. Siyo lazima kutumia nyimbo zote - haya ni mapendekoz tu. Kuimba pia ni njia nzuri ya kuhama kutoka kwenye kipindi kimoja kwenda kwenye kipindi kingine.

Kukusanya Mahitaji ya Kuombea

Usiulizie wala kukusanya mahitaji ya kuombea kutoka

10 SIKU ZA MAOMBI

kwenye kikundi. Badala yake, waambie watu wataje mahitaji yao wakati wanapoomba na kuwahimiza wengine kujiunga wakikubaliana nayo kwa kuungana katika maombi kimya kimya. Sababu kubwa ni Muda! Kuzungumza kuhusu mahitaji ya kila mmoja kunaweza kutumia muda mwingi wa maombi. Shetani anafurahi akiweza kutudumisha katika kuzungumzia tatizo badala ya kuomba kwa ajili ya tatizo hilo. Wanakikundi wanawenza kuanza kushauriana na kupendekeza ufumbuzi. Uwezo unatoka kwa Mungu! Kadiri tunavyoongeza maombi, ndivyo anavyoachia uwezo wakeWake.

Muda Wako wa Kila Siku

Ni wa muhimu sana! Hakikisha wewe kama kiongozi unatumia muda wako mwingi miguuni pa Yesu, ukizungumza naye Naye na kusoma Neno lakeLake. Ikiwa utafanya kumfahamu Mungu kuwa kipaumbele katika Maisha yako, utafunguliwa uzoefu ulio mzuri wa ajabu. "Kutoka katika sehemu ya siri ya maombi ilitoka Nguvu ya ajabu iliyotikisa dunia na kuleta Matengenezo Makuu. Hapo, kwa utulivu mtakatifu, watumishi wa Bwana waliweka miguu yao katika mwamba wa ahadi zake" (*The Great Controversy*, uk. 210). Kiongozi anapoomba, Mungu hushughulika na mioyo!

Utangulizi

Karibu katika Siku Kumi za Maombi 2024! Tunaamini kuwa, katika maombi ndipo mahali uamsho unapozaliwa. Mungu ametenda miujiza mingi katika miaka iliyopita kadiri tulivyokuwa tukimtafuta kwa kuomba na kufunga. Roho Mtakatifu amewezesha uamsho, mabadiliko, hisia za uinjilisti zilizojengwa upya, makanisa yaliyoamshwa, na mahusiano yaliyoponywa. Hapa kuna baadhi ya shuhuda katika miaka iliyopita:

“Kamwe sijawahi kuhisi mguso wa Roho wa Mungu kwa namna hii hapo kabla.” (**Frank B.**)

“Mungu ameiokoa familia yangu kwa njia yakupitia Siku 10 za Maombi” (**Adebayo O.**)

“Wakati wa Siku Kumi za Maombi, niliiombea familia yangu isiyoamini. Katika siku ya 9, mjukuu wangu mwenye umri wa miaka 20 alikuja, na kwa mara ya kwanza kabisa maishani mwake, alianza kuniuliza maswali ya kiroho. Hakika hili lilikuwa jibu la maombi yangu!” (**Fran J.**)

“Tulimwombea baba yangu, ambaye alikuwa ametelekeza imani na sisi kama familia, ili kutafuta wokovu. Mwishoni mwa siku kumi za maombi, kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi, alikuja nyumbani na kuomba msamaha, akitafuta kupatana na akitaka kuweka mambo sawa na Mungu.”? (**G.M.**)

Je, sauti ya Mungu imekuwa ikikuita katika uamsho? Biblia imejaa ahadi kwa ajili yako:

“Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao” (2 Nyakati 7:14).

10 SIKU ZA MAOMBI

“Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote” (Yeremia 29:13).

“Na itakuwa ya kwamba mtu awaye yote atakayeliita jina la Bwana ataponywa” (Yoeli 2:32).

“Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi” (Yakobo 4:8).

“Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami” (Ufunuo 3:20). Po pote ulipo katika maisha sasa, Mungu yupo karibu zaidi kuliko unavyofikiri. Anataka kumwaga mibaraka yake Yake kwa familia yako, kanisa lako, jamii yako, na kwa ulimwengu wako!

Mada yetu ya Maombi: Vipaumbele vya Imani – Maadili ya Kikristo katika Nyakati za Misukosuko

Je! Unajikuta kukamatika katika shughuli za maisha, ukiacha nafasi kidogo tu kwa ajili ya wakati wa kiroho? Ikiwa unatamani maisha ya kiroho yenyе maana zaidi na yenyе utimilifu, Siku hizi 10 za Maombi na tafakari zitakuwa za thamani kwako.

Katika siku hizi kumi, utakuwa na fursa ya pekee ya kuachilia mambo ambayo yanayohusu akili na maisha yako lakini hayaleti kuridhika kwa kweli. Badala yake, tutalenga hasa kaza fikira katika mambo ya maana sana kwa Mungu. Ni nafasi ya kuishi na vitu vichache kimakusudi, ili kukuruhusu upate uzoefu zaidi wa kile ambacho ni muhimu sana.

Katika safari hii yote, utapata utambuzi wa kivitendo ili kuimarisha imani yako kwa Mungu, kuboresha uzoefu wako wa Sabato, na kuimarisha uhusiano wako wa kila siku na Yeye. Maombi yenyе maana, matendo ya fadhili, na kusitawisha shukrani pia yatakuwa sehemu ya

10 SIKU ZA MAOMBI

uchunguzi wetu. Zaidi ya hayo, utapata dhamira, shauku, na ustahimilivu vinavyohitajika ili kufanikiwa.

Hebu tufungue mioyo na akili zetu kwa Mungu, tukimkaribisha Roho wake Wake Mtakatifu kuingia maishani mwetu katika siku hizi kumi. Kupitia mchakato huu, tunaomba ili kubadilishwa na kufanywa upya, ili kuwa mashahidi wenyewe nguvu wa upendo wa Mungu ubadilishao maisha.

Hebu tuombe pamoja kwa ajili ya uamsho wa madhabahu za ibada zetu binafsi na za familia, ili kwamba Roho Mtakatifu aweze kututengeneza upya na kututia nguvu ili tuweze kutangaza ujumbe wa mwisho wa Mungu wa tumaini kwa ulmwengu!

— Dr. Frank Hasel (Mwandishi wa Somo la mwaka huu)

Mwongozo Unaopendekezwa Wakati wa Maombi

- Jitahidi kufanya maombi yawe mafupi – sentensi moja au mbili zilizojenjeka katika mada husika. Kisha wape nafasi wengine. Unaweza kuomba mara nyingi kadiri unavyojisikia, kwa namna ile ile unayozungumza katika mazungumzo.
- Usiogope kuwa kimyaUsitishwe na ukimya, kwani ukimya unampatia kila mmoja muda wa kumsikiliza Roho Mtakatifu.
- Kuimba nyimbo pamoja kadiri Roho Mtakatifu atakavyowaongoza ni mbaraka mkubwa. Hamhitaji kinanda ili kuwaongoza; kuimba bila ala ya mziki ni sawa pia.
- Badala ya kutumia muda wa thamani wa maombi ukizungumza kuhusu mahitaji yako ya kuombea, ni vyema uyaombee tu. Kisha wengine pia wanaweza kuombea mahitaji yako na kudai ahadi kwa ajili ya mahitaji yako.

Kudai Ahadi

Ni faida kwetu kudai ahadi za Mungu katika maombi yetu. Maagizo yote ya Mungu na mashauri yake pia ni ahadi. Hawezi kudai kutoka kwetu jambo fulani ambalo hatuwezi kufanya kwa uweza wakeWake.

Tunapoomba, ni rahisi kujielekeza katika mahitaji yetu, magumu yetu, changamoto zetu - na hasa kulalamika na kulaumu katika maombi kuhusu hali tuliyo nayo. Hili silo kusudi la maombi. Kusudi kubwa la maombi ni kuimarisha imani yetu. Ndiyo maana tunakuhimiza kudai ahadi za Mungu katika muda wako wa maombi. Hamisha macho yako kutoka katika mahitaji yako na changamoto zako na kuyaelekeza kwa Yesu Kristo. Ni kwa kumwangalia yeze Yeye pekee ndipo tunapobadilishwa na kuchukua sura yakeYake.

Ellen White anatutia nguvu kwamba: "Kila ahadi katika Neno la Mungu ni kwa ajili yetu. Katika maombi yako, wasilisha neno lililoahidiwa la Yehova udai kwa imani ahadi zakeZake. Neno lake Lake linatupatia uhakika kwamba ukiomba kwa imani, utapokea mibaraka yote ya kiroho. Endelea kuomba nawe utapata zaidi ya yale uyaombayo au uyawazayo." (In Heavenly Places, uk. 71). Ni kwa namna gani unaweza kudai hizo ahadi za Mungu? Kwa mfano, unapoomba kwa ajili ya amani, unaweza kudai Yohana 14:27 na kusema kuwa, "Bwana umetuambia katika Maandiko yako Yako kwamba 'Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike miyoni mwenu, wala msiwe na woga.' Ninakuomba unipatie amani uliyoahidi kutuachia." Kisha mshukuru Bwana kwamba atakupatia hiyo amani hata kama haujisikii kuwa na amani wakati huo.

Kufunga

Tunakuhamasisha kufanya Mfundo kama ule wa Danieli katika Siku hizi Kumi. Kuanza mwaka kwa maombi ya kufunga ni njia bora ya kuweka wakfu maisha yetu kwa Mungu kwa mwaka unaoanza. Ellen White anatuambia kuwa, "Sasa na kuendelea hata mwisho wa wakati watu wa Mungu wanapaswa kuwa na bidii zaidi, kuwa macho zaidi, kutokuamini hekima yao wenyewe, lakini kuamini hekima ya kiongozi wao, ambaye ni Yesu. Wanapaswa kutenga siku kwa ajili ya kufunga na kuomba. Kujitenga kabisa na chakula kunaweza kusiwe lazima, lakini wanapaswa kula vyakula rahisi zaidi" (*Counsels on Diet and Foods*, uk. 188, 189).

Tunafahamu kuhusu Danieli, aliyekula matunda na mboga mboga kwa siku kumi. Sisi pia tunakuhamasisha kuwa na mlo rahisi sana katika siku hizi kumi. Kama tunataka akili zilizo wazi zaidi ili kuisikia sauti ya Mungu, na kama tunataka kuwa karibu zaidi na MungiMungu, tunahitaji kuhakikisha kwamba chakula chetu hakiwi kikwazo.

Kufunga si kujitenga tu na chakula. Tunakuhamasisha pia kufunga kutazama televisheni, filamu, michezo ya kompyuta, na hata Facebook na YouTube. Wakati mwingine vitu visivyo vibaya, kama Facebook na YouTube, huweza kutuchukulia muda mwingi sana. Weka kando kila kinachowezekana ili uwe na muda mwingi wa kukaa na Bwana.

Kufunga siyo namna ya haraka ya kupata mibaraka kutoka kwa Mungu. Kufunga ni kujinyenyekeza wenyewe ili kwamba Mungu aweze kufanya kazi ndani yetu na kupitia kwetu. Hebu na tusogee karibu naye kupitia maombi ya kufunga, naye atasogea karibu zaidi nasi.

Roho Mtakatifu

Hakikisha unamuomba Roho Mtakatifu akuonyeshe unachopaswa kuombea katika maisha ya mtu fulani, au katika hali fulani. Biblia inatuambia kwamba hatujui tuombee nini na kwamba Roho Mtakatifu ndiye anayetuombea.

“Hatupaswi kuomba tu kwa jina la Kristo, lakini kwa msukumo wa Roho Mtakatifu. Hii huelezea maana ya maneno kwamba Roho “hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.” (Warumi 8:26). Ombi kama hilo Mungu hufurahia kulijibu. Tunapoomba kwa dhati na kwa nguvu tunaomba kwa jina la Kristo, katika nguvu hiyo kuna ahadi kutoka kwa Mungu kwamba anakaribia kujibu maombi yetu ‘zaidi ya tuyaoombayo au tuyawazayo’ (Waefeso 3:20” (*Christ Object Lessons*, uk. 147).

Imani

Tunasoma katika Roho ya Unabii kwamba “maombi na imani vitafanya kile ambacho hakuna nguvu duniani inachowenza kufanya” (The Ministry of Healing, uk. 509). Pia tunaambiwa kwamba “ahadi yo yote aliyoahidi, tunaweza kuiomba; kisha tunapaswa kuamini kwamba tumeipokea, na kurudisha shukrani kwa Mungu kwamba tumepokea” (Education, uk. 258). Hivyo jenga tabia ya kumshukuru Mungu kwa imani kabla kwa kile atakachotenda na namna atakavyojibu maombi yako.

Ombea Wengine

Katika siku hizi kumi tunakuhimiza kuombea watu ambaeo Mungu amewaweka katika maisha yako kwa namna ya pekee. Chagua watu watano hadi saba - wanaweza kuwa ndugu, marafiki, wafanyakazi wenzako, majirani, au hata watu unaowafahamu tu. Tenga muda kumuuliza Mungu kuwa, angependa umuombee nani. Mwombe pia akupatie

10 SIKU ZA MAOMBI

mzigo halisi wa watu hawa. Andika majina yao kwenye karatasi na uitunze sehemu salama, kama kwenye Biblia yako. Utashangazwa namna Mungu anavyofanya kazi katika kujibu maombi yako!

Changamoto ya Kuwafikia Watu walio Nje ndani ya Siku Kumi za Maombi

Yesu hatuuti kwa ajili ya kuomba tu bali anatuita ili pia, kuhudumia mahitaji ya wale wanaotuzunguka. "Kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia" (Mathayo 25:35, 36).

Katika kitabu cha *Huduma ya Uponyaji* (*The Ministry of Healing*) tunasoma kuwa, "Tunapaswa kuishi maisha yenye sura mbili – maisha ya mawazo na matendo, na maisha ya maombi ya kimya na kazi inayofanywa kwa juhudii" (uk. 512). Tumepokea upendo mwingi sana kutoka kwa Mwokozi wetu; na tuna fursa ya kushiriki upendo huo na marafiki, majirani, hata watu tusiowafahamu wenye uhitaji.

Muulize Mungu katika maombi namna bora ya kuwafikia wengine katika Siku hizi Kumi za Maombi. Unapokuwa ukifanya kazi ya kupanga kila kitu, epuka kuruhusu shughuli hizo kukufanya ushindwe kuomba. "Jitihada binafsi kwa ajili ya wengine zinapaswakwanza kutanguliwa na maombi mengi ya faragha; kwani hekima kubwa inahitajika ili kuelewa sayansi ya kuokoa roho. Kabla ya kuwasiliana na watu, wasiliana na Kristo. Pata maandalizi ya kuhudumia watu kutoka katika kiti cha enzi cha neema ya kimbingu." (Maombi, uk. 313).

Katika nyenzo za Siku Kumi za Maombi mtandaoni, utapata nyaraka iliyojaa mapendekezo mengi ya kuwafikia wengine. Yesu anakualika kuwa mikono na miguu yake Yake kwa ulimwengu wenye uhitaji!

Kuhusu Mwandishi

Frank M. Hasel, Ph.D., ni mwanatheolojia na mwandishi ambaye anatumika kama Mkurugenzi Mshiriki wa Taasisi ya Utafiti wa Kibiblia (BRI) katika Makao Makuu ya Ulimwengu ya Kanisa la Waadventista wa Sabato wa Sabato huko Silver Spring, MD. Katika kitabu chake kipyta, *Love Is! A Journey of Grief, Grace, and Gratitude* (Cascade, 2024), anashiriki wazi uzoefu wake binafsi wa kumpoteza mke wake mpendwa kutokana na saratani, akitoa maarifa muhimu kuhusu hali ya huzuni na maana ya kupitia hasara kubwa maishani.

Akiwa mzaliwa wa Ujerumani, alihudumu kama mchungaji aliyewekewa mikono, mwalimu wa Biblia, na mkuu wa kitivo cha teolojia huko Ulaya kabla ya kuhamia Marekani. Frank anafurahia sana uhusiano wake na Yesu, anafurahia mazungumzo yanayoamsha fikra, anathamini wema wa kweli, anapata faraja katika kutembelea maeneo ya asili, na anafurahia mara kwa mara aiskrimu isiyo na maziwa.

Frank anaamini kabisa kwamba mafundisho ya Biblia yana ufunguo wa kustawi kwa wanadamu, yakiboresha kila kipengele cha maisha. Ili kuendelea kuwasiliana naye, unaweza kufuata safari yake kwenye Instagram (@frank.m.hasel) na Facebook (<https://www.facebook.com/Frank.M.Hasel>), au tembelea tovuti yake www.frankmhasel.com

Masomo haya yameandaliwa na Idara ya Huduma, Konferensi Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato.

Isipokuwa ilipoelezwa, nukuu zote zinatoka katika toleo la Biblia la “Swahili Union Bible” © 1997

USIKU WA MAOMBI:

Fikiria kuandaa huduma ya maombi ya usiku mzima kama sehemu ya Siku Kumi za Maombi. Kwa mfano, unaweza kuanza saa 12 jioni na kumaliza saa 12 asubuhi. Chagua ratiba itakayofaa kwa kundi lako.

Kwa nini kuwa na Usiku wa Maombi?

Hakuna chochote “kitakatifu” katika kukaa macho huku ukiomba usiku kucha. Hata hivyo, ni kweli kwamba usiku unaweza kuwa ni wakati wa pekee ambao watu hawana mambo mengi ya kufanya au kuwa katika hali ya haraka. Tunaamini kwamba lengo lako halipaswi kuwa kukaa macho usiku kucha, bali ni kuomba sana kadiri inavyohitajika hadi utakapokuwa umeombea vitu vyote unavyohisi kwamba Mungu anataka uviombee.

Tunapendekeza kwamba baadhi ya watu waongoze usiku huo. Hakikisha kunakuwa na mapumziko. Kama kiongozi, unaweza kuona hali ilivyo na kufahamu wakati mapumziko yanapohitajika na wakati utakapoona inafaa kuhamia katika kipengele kinachofuata cha maombi. Unaweza pia kuingiza usomaji wa vifungu vya Biblia katika muda wako wa maombi. Unaweza kufanya mambo yote yaliyopendekezwa au baadhi yake, inategemea kile kilicho bora kwa kikundi chako. Kuwa huru kubadilisha mtiririko kadiri utakavyoona inafaa.

Mapendekezo ya Mpangilio wa Usiku wa Maombi

- *Anza kwa kipindi cha sifa.* Msifu Mungu katika maombi yako na pia kupitia nyimbo.
- *Tumia muda kwa ajili ya kuungama,* ukihakikisha kwamba hakuna kinachomzuia Mungu kusikia maombi yako. Wapatie watu muda wa maungamo binafsi na weka muda wa kuungama kwa pamoja. Hamasisha watu kuungama dhambi zao binafsi

10 SIKU ZA MAOMBI

wakiwa peke yao na kuungama dhambi za wazi kwa uwazi. Katika Danieli 9:1-19 tunasoma kumhusu Danieli, aliyeomba na kuungama kwa wazi dhambi za watu wa Mungu.

- *Ombea mahitaji ya watu walio katika mkutano huo wa maombi.* Watu wengi wanaumia au wana uhitaji wa maombi, au wanamfahamu mtu mwenye uhitaji wa maombi. Tengeneza duara, weka kiti katikati, na alika wale wenye maombi maalumu waje mmoja baada ya mwingine na kushiriki maombi yao. Kisha kusanyikeni kumzunguka mtu huyu na waruhusu watu wawili au watatu kuomba kwa ajili ya mahitaji mahususi ya mtu huyo na kudai ahadi za Mungu.
- *Gawa kikundi katika vikundi viwili vidogo.* Waruhusu wanawake kuomba katika chumba kimoja (wakiwa na kiongozi wa kike) na wanaume katika chumba kingine (wakiwa na kiongozi wa kiume). Mahitaji mengi binafsi hayawezi na hayapaswi kushirikishwa na kila mtu. Ni rahisi zaidi kushiriki pamoja na wale wa jinsia moja.
- *Baada ya kurudi pamoja, ombea mahitaji ya jamii na kanisa lenu.* Pia tumia muda kwa ajili ya **maombi ya kanisa la ulimwengu** (yaliyoorodheshwa katika ukurasa wa maombi ya kanisa la kiulimwengu). Siyo lazima kumaliza orodha nzima ya maombi, kwa hiyo usiharakishe ukiwa na hisia za kutaka kumaliza orodha yote. Unaweza kugawa maombi katika vikundi vidogo vidogo na kuwapatia kila kikundi sehemu ya orodha hiyo.
- *Ombea orodha ya watu watano hadi saba uliokuwa ukiwaombea katika siku hizi kumi*
- *Chagua kifungu cha Biblia na kuombea.*
- *Funga muda wa maombi kwa kipindi kingine cha kusifu na kushukuru.*

Changamoto za Kuwafikia watu walio nje Ndani ya Siku Kumi za Maombi

Yesu hatuiti kwa ajili ya kuomba tu bali anatuita pia ili kuhudumia mahitaji ya wale wanaotuzunguka. "Kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia" (Mathayo 25:35, 36).

Katika kitabu cha *Huduma ya Uponyaji* (*The Ministry of Healing*) tunasoma kuwa, "Tunapaswa kuishi maisha yenye sura mbili - maisha ya mawazo na matendo, na maisha ya maombi ya kimya na kazi inayofanywa kwa juhudii" (uk. 512). Tumepokea upendo mwingi sana kutoka kwa Mwokozi wetu; na tuna fursa ya kushiriki upendo huo na marafiki, majirani, hata watu tusiowafahamu wenye uhitaji.

Muulize Mungu katika maombi namna bora ya kuwafikia wengine katika Siku hizi Kumi za Maombi. Unapokuwa ukifanya kazi ya kupanga kila kitu, epuka kuruhusu shughuli hizo kukufanya ushindwe kuomba. "Jitihada binafsi kwa ajili ya wengine zinapaswa kwanza kutanguliwa na maombi mengi ya faragha; kwani hekima kubwa inahitajika ili kuelewa sayansi ya kuokoa roho. Kabla ya kuwasiliana na watu, wasiliana na Kristo. Pata maandalizi ya kuhudumia watu kutoka katika kiti cha enzi cha neema ya kimbingu." (*Maombi*, uk. 313).

Hapa kuna baadhi ya njia unazoweza kutumia kusaidia wengine. Chagua njia yo yote utakayoona inakidhi mahitaji ya wale unaokwenda kuwashudumia, na jisikie huru kuongeza mawazo yako.

- Mpikie mgonjwa chakula.
- Mkaribishe jirani/mfanyakazi mwenzako kwenye kusanyiko la kijamii.

10 SIKU ZA MAOMBI

- Mpatie chakula mtu asiye na makazi.
- Tafuta mzee mmoja. Mtembelee kila siku na umsaidie kazi, kama vile kumnunulia mahitaji, kumpikia, au kumsaidia kazi za bustani, n.k.
- Oka mkate na ushiriki huo mkate na jirani.
- Saidia kwenye miradi katika maeneo yanayokuzunguka.
- Jitolee kukaa na mgonjwa au mtu asiyejiweza ili wale wanaomhudumia waweze kufanya shughuli zingine.
- Jitambulisse kwa jirani mpya aliyehamia maeneo yenu na kumpelekea chakula. Mfanye ajisikie kukaribishwa katika maeneo hayo.
- Nunua mahitaji ya jikoni na upelekee familia yenye uhitaji.
- Toa msaada miwani yako ya zamani.
- Jitolee kutoa masomo ya Biblia
- Tembelea sehemu za kutunzia watu wenye uhitaji na kuwafariji.
- Mpatie mwanafunzi fedha ya “chakula.”
- Kusanya nguo kwa ajili ya wahitaji. Unaweza kuanzisha kabati la nguo kanisani kwako kwa ajili ya kushirki na wale walio na uhitaji.
- Toa msaada kompyuta yako au vifaa vingine vya kielektroniki usivyotumia.
- Toa msaada gari lako lililotumika.
- Andaa “Tamasha la Kupima Afya.”
- Tuma kadi kwa mtu aliyefungiwa ndani.
- Andaa mfululizo wa mambo ya uinjilisti.
- Mpatie mtu kitabu unachodhani angekipenda.
- Wapigie simu jirani zako na kuwajulia hali.
- Gawa vijarida na vijuzuu kwa watu. Vinapatiakana kwenye tovuti ifuatayo hapa: www.glowonline.org/glow
- Mwalike mtu kumpokea Yesu.
- Endesha darasa la mapishi.

10 SIKU ZA MAOMBI

- Fanya "Mradi wa machapisho 28." Katika Juma la kwanza, gawa kitabu kimoja. Juma la pili, gawa vitabu viwili. Juma la tatu, gawa vitabu vitatu. Endelea hadi utakapogawa vitabu vyote 28.
- Mpelekee chakula mtu aliye poteza (aliyefiwa na mpendwa wake).
- Mtembelee mtu hospitali ili kumtia moyo au kumsaidia kwa namna moja au ny ingine.
- Msomee mzee kitabu.
- Tembelea makazi ya watoto yatima pamoja na wanaoishi katika mazingira magumu na toa msaada kwa wafanyakazi wa hapo.
- Anza kundi la kushona/kufuma ili kutengeneza nguo kwa ajili ya wahitaji.
- Msomee Biblia kwa sauti mtu asiyeona au asiyeweza kusoma.
- Endesha usiku wa vijana nyumbani kwako.
- Toa makazi kwa watu walionyanyaswa.
- Gawa baadhi ya vitabu kwenye makazi ya watoto.
- Panga na kusimamia siku ya kufurahi kwa ajili ya watoto na wenyewe mahitaji maalumu pamoja na familia zao.
- Andaa siku ya kufanya usafi katika jamii.
- Anzisha chama cha afya katika kanisa lako. Alikar marafiki na majirani.
- Muulize mtu kama angependa kuungana na wewe kutazama mkanda wenyewe ujumbe wa kiroho. Kadiri mnavyotazama pamoja, omba kwamba Roho Mtakatifu anene na moyo wa mtu huyo.
- Buni mradi wako mwenyewe.

Kwa vitendea kazi zaidi juu ya ushuhudiaji, tembelea tovuti ifuatayao: www.revivalandreformation.org/resources/witnessing.

Ahadi za Biblia za Kudai kwenye Maombi

Ahadi za Roho Mtakatifu

“Mwombeni Bwana mvua wakati wa masika, naam, Bwana afanyaye umeme, naye atawapa manyunu ya mvua, kila mtu atapewa nyasi kondeni.” Zakaria 10:1

“Basi, ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?” Luka 11:13

“Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia... Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.” Yohana 14:26; 16:8

“Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, ye ye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya.” Yohana 14:12 – 14

“Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la Bwana kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi.” Zakaria 4:6

Ahadi kwamba Mungu Hujibu Maombi

“Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.” Yohana 15:7

“Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.” Waebrania 4:16

10 SIKU ZA MAOMBI

"Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24

"Ukaniite siku ya mateso; Nitakuokoa, na wewe utanitukuza." Zaburi 50:15

"Tenanawaambia,yakwambawiliwenuwatakopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni." Mathayo 18:19

"Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea." Mathayo 21:22

"Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya." Yohana 14:13, 14

"Tena siku ile hamtaniuliza neno lo lote. Amin, amin, nawaambia, Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu." Yohana 16:23, 24

"Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba." 1 Yohana 5:14, 15

Ahadi kuhusu Nguvu ya Mungu

"Kuna neno gani lililo gumu la kumshinda Bwana? Kwa muhula wake nitakurudia, wakati huu huu mwakani, na Sara atapata mwana wa kiume." Mwanzo 18:14

"Bwana atawapigania ninyi, nanyi mtanyamaza kimya." Kutoka 14:14

"Yesu akawakazia macho, akasema, Kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu sivyo; maana yote yawezekana kwa Mungu." Marko 10:27

10 SIKU ZA MAOMBI

"Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya." 1
Wathesalonike 5:24

"Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, Na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuulika." Ayubu 42:2

"Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu? Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?"
Warumi 8:31, 32

"Mungu si mtu, aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute; Iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo amenena, hatalifikiliza?" Hesabu 23:19

"Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki; akili zake hazichunguziki. Huwapa nguvu wazimiao, humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo. Hata vijana watazimia na kuchoka, na wanaume vijana wataanguka; bali wao wamnganjeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia." Isaya 40:28 - 31

Ahadi za Uongozi wa Mungu

"Je! Si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako." Yoshua 1:9

"Na tazama, mimi nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia."
Mwanzo 28:15

"Tazama, mimi namtuma malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengezea." Kutoka 23:20

10 SIKU ZA MAOMBI

“Lakini huko, kama mkimtafuta Bwana, Mungu wako, utampata, ukimtafuta kwa moyo wako wote, na roho yako yote.” Torati 4:29

“Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua.” Yeremia 33:3

“Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; Palipopotoka patakuwa pamenyoka, Na palipoparuza patasawazishwa; Na utukufu wa Bwana utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja; Kwa kuwa kinywa cha Bwana kimenena haya.” Isaya 40:4, 5

“Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; Nitakushauri, jicho langu likikutazama.” Zaburi 32:8

“Naye Bwana, ye ye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaike.” Torati 31:8

“Ni nani amchaye Bwana? Atamfundisha katika njia anayoichagua.” Zaburi 25:12

“Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri ye ye, Naye atayanyosha mapito yako.” Mithali 3:5, 6

“Na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.” Isaya 58:10, 11

“Nao watatoka nje na kuitazama mizoga ya watu walioniasi; maana funza wao hatakufa, wala moto wao hautazimika

10 SIKU ZA MAOMBI

nao watakuwa chukizo machoni pa wote wenye mwili.”
Isaya 65:24

Ahadi za Moyo Uliobadilishwa

“Nami nitawapa moyo, wanijue ya kuwa mimi ni Bwana; nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao; kwa maana watanirudia kwa moyo wao wote.” Yeremia 24:7

“Bwana, Mungu wako, atautahiri moyo wako, na moyo wa uzao wako, ili umpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, upate kuwa hai.” Torati 30:6

“Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama.” Ezekieli 36:26

“Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema miyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu;” Wafilipi 1:6

“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipyta; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.” 1 Wakorintho 5:17

“Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.” Wagalatia 2:20

“Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya.” 1 Wathesalonike 5:23, 24

10 SIKU ZA MAOMBI

Ahadi za Msamaha

“Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao.” 1 Nyakati 7:14

“Kwa maana Wewe, Bwana, U mwema, Umekuwa tayari kusamehe, Na mwingi wa fadhilli, Kwa watu wote wakuitao.” Zaburi 86:5

“Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu.” Marko 11:25

“Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.” Waefeso 4:32

“Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.” 1 Yohana 1:9

“Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluiji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.” Isaya 1:18

“Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako.” Isaya 43:25

“Maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena.” Yeremia 31:34

“Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.” Waefeso 1:7

10 SIKU ZA MAOMBI

Ahadi za Ushindi Dhidi ya Dhambi

“Kwa maana kila kitu kilichozaaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu.” 1 Yohana 5:4

“Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeze aliyetupenda.” Warumi 8:37

“Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” 1 Wakorintho 15:57

“Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuumi wa haki yangu.” Isaya 41:10

“Zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu.” Waefeso 6:16

“Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.” Wagalatia 2:20

“Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.” Wafilipi 2:13

“Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.” Wagalatia 5:16

“Naye Mungu wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja nanyi. Amina.” Warumi 16:20

“Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi

10 SIKU ZA MAOMBI

ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.”
Warumi 12:2

“Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia.
Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani
yake.” 1 Yohana 2:15

Ahadi za Uponyaji

“Akawaambia, Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya
Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele
zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuzishika
amri zake, mimi sitatia juu yako maradhi yo yote niliyowatia
Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye.”
Kutoka 15:20

“Makomeo yako yatakuwa ya chuma na shaba; Na kadiri
ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako.” Torati
33:25

“Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, Wala usizisahau fadhili
Zake zote. Akusamehe maovu yako yote, Akuponya
magonjwa yako yote, Aukomboa uhai wako na kaburi,
Akutia taji ya fadhili na rehema, Aushibisha mema uzee
wako, Ujana wako ukarejezwa kama tai.” Zaburi 103:2 - 5

“Usiwe mwenye hekima machoni pako; Mche Bwana,
ukajiepushe na uovu. Itakuwa afya mwilini pako, Na
mafuta mifupani mwako.” Mithali 3:7, 8

“Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni
nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha
nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.
Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni
zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa
na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu,
Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu
ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.”
Isaya 53:3-5

10 SIKU ZA MAOMBI

“Uniponye, Ee Bwana, nami nitaponyeka; uniokoe, nami nitaokoka; kwa maana wewe ndiwe uliye sifa zangu.” Yeremia 17:14

“Maana nitakurudishia afya, nami nitakuponya jeraha zako, asema Bwana, kwa sababu wamekuita, mwenye kutupwa, wakisema, Ni Sayuni, ambao hapana mtu autakaye.” Yeremia 30:17

“Tazama, nitauletea afya na kupona, nami nitawaponya; nami nitawafunulia wingi wa amani na kweli.” Yeremia 33:6

“Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu, jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake; nanyi mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa mazizini.” Malaki 4:2

“Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa.” Yakobo 5:14, 15

Ahadi kwa ajili ya Nguvu za Kufanya Mapenzi ya Mungu “Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanya utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.” 2 Wakorintho 4:16-18

“Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.” Wagalatia 6:9

“Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.” Wafilipi 4:13

10 SIKU ZA MAOMBI

"Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema." Wafilipi 2:13

"Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu." 2 Wakorintho 12:9

Ahadi Kuhusu Kuwa Mashahidi wa Mungu

"Msiogope wala msifanye hofu; je! Sikukuhubiri haya zamani na kuyaonyesha? Na ninyi ni mashahidi wangu. Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba; mimi sijui mwingine." Isaya 44:8

"Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia." Isaya 60:1

"Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho." 2 Wakorintho 5:18

"Lakini Bwana akaniambia, Usiseme, Mimi ni mtoto; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru." Yeremia 1:7

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." Matendo 1:8

"Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeche aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu." 1 Petro 2:9

"Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu." 1 Petro 3:15

Sherehe ya Siku ya Sabato

Andaa Sabato ya Mwisho ya Siku Kumi za Maombi kwa namna ya kusherehekeea wema wa Mungu na nguvu yake kuu. Shiriki namna ulivyopata uzoefu wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu katika siku hizi kumi zilizopita. Sherehekeea mambo yale Mungu aliyotenda, anayotenda, na atakayotenda.

Mahitaji ya kila kusanyiko yanatofautiana, hivyo tafadhali fanya kazi pamoja na viongozi wa kanisa mahalia ili kuandaa mpango mahususi kwa ajili ya kanisa lako. Hapa kuna baadhi ya mambo ya kujumuisha katika ibada ya kanisa lako katika Sabato ya Mwisho.

Wazo Kuu:

Vipaumbele vyta Imani: Maadili ya Kikristo katika Nyakati za Misukosuko

Fungu Elekezi:

“Ee mwanadamu, ye ye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako!”
(Mika 6:8)

Mapendeleko ya Nyimbo:

- Wimbo wa Maandiko Mika 6:8.
- Moyo Safi. No. 116
- Bwana, Nami. No. 61
- Jaza Kikombe Changu. No 287. (VV)
- Furaha Gani! No. 43/251
- Yote Namtolea Yesu. No. 122/332

Mapendeleko ya Hubiri

Hebu mchungaji, mzee, au kiongozi wa maombi ahubiri hubiri kuhusu baadhi ya maadili ya Kikristo yaliyoangaziwa katika masomo ya Maombi ya Siku Kumi mwaka huu 2024.

10 SIKU ZA MAOMBI

[AU]

Hebu wale walioshiriki katika Siku Kumi za Maombi wapeane kutoa muhtasari mfupi (dakika 1-2) kwa kila mwongozo wa siku 10 za maombi ya kila siku. Wasilisha kichwa, fungu kuu, na wazo kuu. (Jiandaeni mapema ili muhtasari ubakie ndani ya dakika 1-2. Kwa watu wengi, dakika moja ni maneno 125-150 yanayozungumzwa.)

[AU]

Orodhesha washiriki watatu wa vikundi vyta umri tofauti tofauti ili kutoa mawasilisho mafupi (dakika 5-10) kuhusu jinsi wanavyoishi kimakusudi maisha ya Kikristo na yenye maana kila siku.

Hitimisha kwa kutoa wito kwa wasikilizaji kufanya matembezi yao ya Kikristo kuwa yale yaliyokitwa katika Kristo zaidi, katika kibiblia, na yenye maana kulingana na wema na maadili katika usomaji wa Siku Kumi za Maombi.

Mawazo Mengine ya Programu:

Shuhuda za washiriki juu ya maombi yaliyojibiwa, Muda wa maombi ya vikundi vidogo, Matangazo ya maombi na shughuli zijazo za huduma, Kisa cha watoto kuhusu maombi, Chaguzi za nyimbo maalumu, etc.

Mahitaji ya Kuombewa kwa kanisa la ulimwengu

1. Bwana, tunaomba uruhusu ule uamsho wa ucha Mungu wa zamani ulikumbe kanisa Lako katika siku hizi za mwisho. Tuwezeshe kusimama hata kama mbingu zianguke. Ruhusu uamsho huu uanze na mimi.
2. Bwana tunaomba utuweze kuwa thabiti katika maombi kila siku, kwa mtu binafsi na kwa familia.
3. Bwana, tunaomba utufungue macho yetu ili ktuona uharibifu maishani mwetu. Mambo ambayo yanatuzuia tusiweze kukaza macho yetu Kwako. Tupatie miyo ya kupenda kukuabudu Wewe tu.
4. Bwana, tunaomba utusaidie tukuruhusu Wewe kutuamsha kila siku asubuhi, bila kujali ni mapema kiasi gani, ili kwamba tuweze kuwa, na muda mzuri pasipo haraka katika Neno Lako na maombi.
5. Tunaomba kwamba utuwezeshe kukujia jinsi tulivyo, kwa hisia zetu zote, mapungufu yetu, dhambi zetu, na mahitaji yetu, na tukuruhusu Utupende, utubadilishe na kutuumba upya ukitufanya kuwa vile Upendavyo tuwe.
6. Bwana, tufundishe namna ya kuomba kila siku kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu.
7. Tunaomba kwa ajili ya mvua ya masika ya Roho Mtakatifu ili kuimarisha ushuhudiaji wetu na kutuwezesha ili kujihusisha katika kazi ambayo Umetupatia kabla ya ujio Wako.
8. Tufundishe jinsi ya kuzipenda familia zetu kwa kujitoa kafara na namna ya kuwafanya wanafunzi kwa ajili ya Ufalme, kuanzia kwa watoto wetu na wapendwa wetu.
9. Tunaomba utupatie hekima ya kulichunguza, kulielewa na kilitii Neno la Mungu. Tunaomba utufundishe kuyapambanua vyema maneno ya

10 SIKU ZA MAOMBI

ukweli na kwa uaminifu kuwashirikisha wengine Neno Lako.

10. Bwana, tunaomba uamshe upya hali yetu ya kuyathamini maagizo yanayopatikana katika maandiko yaliyovuviwa ya Ellen G. White.
11. Tunaomba kwa ajili ya uhuru wa dini, na haki ya dhamiri ulimwenguni kote. Bwana, tunaomba ufungue milango kwa ajili ya utangazwaji wa Neno Lako katika maeneo yaliyofungwa.
12. Bwana, tunaomba kanisa Lako ulimwenguni liitikie wito wa kutangaza ujumbe wa malaika watatu kwa kila taifa, lugha na jamaa. Tuoneshe jinsi ya kukaza mafundisho haya yote katika upendo na haki ya Kristo Yesu.
13. Bwana, tunaomba uwawezeshe Waadventista wa Sabato wote ulimwenguni kuitika "Nitakwenda" na kuuchukua mwito ili kukutumikia na kuhubiri habari njema ya wokovu.
14. Tunaomba kwamba Waadventista wa Sabato wote ulimwenguni wawe tayari kusaidia na kutia moyo wale wote wanaopita katika adha ya maumivu maishani. Tunaomba utupatie ujasiri, ubunifu na roho isiyo na ubinafsi pale jirani zetu wanapokuwa wakituhitaji sana.
15. Tunawaombea wale wote walioathirika kifedha kwa sababu ya mabadiliko ya kiuchumi.
16. Bwana, tunaomba uwaoneshe waumini makanisani namna ya kuwaidia wale ambao wanapambana na matatizo ya afya ya akili au ya kutengwa.
17. Tunawaombea wachungaji pamoja na makanisa kupata namna ya kuwezesha waumini kuomba pamoja kwa bidii. Bwana, tunaomba uliunganishe kanisa Lako pamoja katika ibada na huduma.
18. Tunaomba kwa ajili ya uamsho wa kiroho mionganoni mwa vijana wa kanisa la Waadventista wa Sabato wanaohudhuria katika vyuo vikuu na taasisi nyingine

10 SIKU ZA MAOMBI

za elimu ulimwenguni kote. Tunakuomba Bwana, uwafanye kuwa mabalozi wakereketwa kwa ajili ya Yesu.

19. Tunaombea asilimia 69 ya watu ulimwenguni ambao hawajapokea mafundisho ya Yesu yasiyochafuliwa.
20. Tunaombea watu milioni 62 katika miji 28 ambayo haijafikiwa au imefikiwa kwa uchache katika nchi ya Urusi (Divisheni ya Euro-Asia.)
21. Tunaomba Mungu ainue wamisionari jasiri walio tayari kufanya kazi kati ya makundi 746 yaliyopo katika nchi 20 za Mashariki ya kati.
22. Bwana, tafadhalii uinue wanafunzi Wa-Aldensia ambao wako tayari kukutumikia katika maeneo magumu.
23. Tunawaombea waumini wa kanisa la Waadventista wa Sabato wanaokabiliwa na mateso na kutupwa gerezani kwa sababu ya Imani yao.
24. Tunaomba kwa ajili ya watu milioni 202 waliopo katika miji 41 iliyofikiwa kwa uchache katika Division ya Asia Pacific kusini wapate kumfahamu Yesu.
25. Tunaomba kwa ajili ya Idara ya Shule ya Sabato na Huduma Binafsi ya kila kanisa mahalia kadiri wanavyotafuta mpango wa Mungu na kuwafikia walio nje katika jamii kwa huduma za upendo, mafunzo ya Biblia, na ushuhuda binafsi.
26. Tunaomba kwa ajili ya shirika la misaada la Waadventista wa Sabato (ADRA) kadiri wanavyokabiliana na mahitaji ya watu ulimwenguni kote.
27. Tunawaombea watu milioni 16 katika miji 6 ambayo imefikiwa kwa uchache sana katika divisheni ya Pacific ya kusini.
28. Tunaomba kuwa Roho Mtakatifu atusaidie kufahamu jinsi ya kufikia watu milioni 406 katika miji 105 ya divisheni ya Asia Pacific ya kaskazini ambayo haijafikiwa au imefikiwa kwa uchache sana.

10 SIKU ZA MAOMBI

29. Bwana, tunaomba ubariki Huduma ya Uchaplensi ya kanisa la Waadventista wa Sabato iweze kuhamasisha wahudumu pamoja na waumini wenye shauku ya kuhudumia watu waliopo magerezani.
30. Ee Bwana, tunaombea waalimu wa Shule ya Sabato. Wasaidie kufahamu umuhimu wa kazi yao kwa watoto wetu.
31. Bwana, tunaomba uongozi Wako kwa ajili ya vituo vingi vya mvuto, program za afya na familia, pamoja na chama cha Watafuta njia ulimwenguni kote.
32. Bwana, tunaomba utuoneshe jinsi ya kupeleka machapisho yaliyojawa na kweli kwa jamii zetu. Tunaomba kwamba uwajalie kuyasoma na kwamba Roho Mtakatifu alete ushawishi katika ukweli wa Biblia.
33. Bwana, tunaomba ulinzi wako kwa wamisionari wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi.
34. Tunakuomba uinue wainjilisti wa vitabu, wanafunzi wa kujitolea, waandishi, wataalam wa mitando ya kijamii, pamoja na wafadhili watakaosaidia kueneza maneno ya matumaini na uzima.
35. Tunaomba kwa ajili ya shule za kanisa la Waadventista wa Sabato, wanafunzi, pamoja na waalimu ulimwenguni kote. Hebu shule hizi zifundishe kwa uaminifu kweli za Biblia na kuwaongoza vijana katika utume, huduma na kushiriki uhusiano na Kristo.
36. Bwana, tupatие hekima ya kufikia tamaduni zingine ambazo hazina shauku ya dini. Hebu Roho wako Mtakatifu aangushe kuta ambazo zinazunguka roho hizo.
37. Tunakuomba utubariki kadiri tunavyowaendea watu waliofungwa katika ibada ya mizimu, ibada ya sanamu, na imani katika vitu vinavyoonekana. Tusaidie kuelewa mtazamo wao wa kidunia na kisha ktuwatambulisha kwa Mwokozi wao binafsi.

10 SIKU ZA MAOMBI

38. Bwana, tunakuomba ulete uvuvio kwa kanisa la Waadventista wa Sabato ulimwenguni kote wapate kuomba kwa namna ambayo hawajawahi kuomba. Tufundishe kudai ahadi zako na kutazamia kwamba utahamisha milima zaidi tunapoomba.
39. Tunaomba kwa ajili ya makundi 514 ya watu katika nchi 18 za Divisheni ya Bahari ya Hindi Kusini mwa Afrika. Tafadhali waongoze katika ukweli wa Biblia.
40. Tunakuomba utuoneshe jinsi ya kufikia mahitaji ya kiroho ya wakimbizi. Hebu kanisa letu lifahamike kwa upendo wetu kwa watu wote, bila kujali kuwa ni akina nani au wanatoka wapi.
41. Tunakuomba uinue wamisionari wa mijini wapate kuanzisha makanisa kwa makundi 806 ya watu katika nchi 20 za Divisheni ya Ulaya (Inter—Europe Division.)
42. Tunakuomba uinue jeshi la watendakazi watakaoanzisha makanisa kati ya makundi 948 ya watu katika nchi 38 za Divisheni ya Amerika (Inter—America Division)
43. Bwana, tunakuomba uandae vijana watakaojihusisha katika kuanzisha makanisa kati ya makundi 789 ya watu katika nchi 9 za Divisheni ya Amerika kaskazini.
44. Tunakuomba uandae watu wa kujitolea ili kuhudumia makundi 70 ya watu katika Fildi ya Israeli.
45. Tunakuomba uinue matabibu wa kimisionari ili kuanzisha makanisa kati ya makundi 830 ya watu katika nchi 11 za Divisheni ya Afrika Kati Mashariki.
46. Tunakuomba uinue mashujaa wa maombi wapate kuombea makundi 2,568 ya watu katika nchi 4 za Divisheni ya Asia kusini.
47. Tafadhali wezesha familia zetu kudhihirisha upendo Wako majumbani mwetu na katika jamii zinazotuzunguka. Tunaomba ulete maelewano majumbani, ponya mahusiano yaliyovunjika, linda wahanga wa unyanyasaji, na dhihirisha uwezo Wako

10 SIKU ZA MAOMBI

utakasao katika hali zinazoonekana kutokuwa na matumaini.

48. Tunakuomba uinue wauguzi na madaktari wa kuanzisha makanisa mapya kati ya makundi 1,978 ya watu katika nchi 22 za Divisheni ya Afrika Kati Magharibi.
49. Tunaomba kwa ajili ya watu milioni 49 katika miji 19 ambayo hijafikiwa au imefikiwa kwa uchache sana katika Divisheni ya Trans Europe.
50. Tunaomba kwa ajili ya Watoto wetu. Tafadhali wawezeshe kusimama kwa ujasiri kukutetea wanapokabiliana na vikwazo na misukumo. Wasaidie kufanya chaguzi sahihi na kusimamia ukweli.
51. Tunaomba utufundishe kufuata mfano wa Yesu usiokuwa na ubinafsi kwa kufikia mahitaji ya kila siku ya watu wanaotuzunguka. Tuwezeshe kuhudumu kama wamisionari matabibu, watu wanaojitolea katika jamii, na rafiki za watu wenye uhitaji.

Vipaumbele vya Imani

Siku ya Kwanza

Wingi si Hoja

Fungu Elekezi: “*Basi angalieni sana jinsi mnavyo enenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenyewe hekima; mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu.*” – Efe. 5:15, 16.

Je! Wingi ni Hoja Kweli?

Maisha yetu yamejawa na mambo mengi tunayotaka kuyashughulikia. Katika jamii ambayo inaendeshwa kichaa na ununuzi na uuzaji, tunashawishiwa kwa urahisi kuamini kwamba kadiri tunavyokuwa navyo zaidi, ndivyo tunavyokuwa na furaha. Kwa sababu ya matangazo yenye kuvutia yanayotuzunguka, tunakosea kutamani kuwa navyo vyote. Wakati mwingine tunapanua fikra hizi hata kwa kazi yetu kwa Mungu. Tunataka kumtumikia Mungu, lakini wakati uohuo, hatutaki kukosa kitu kingine chochote kinachopita machoni petu. Na kwa hiyo tunajaribu sana kupatanisha tamaa yetu ya kumtumikia Mungu na utafutaji usio na mwisho wa mambo mengi zaidi na zaidi. Hii inatufanya kuwa na shughuli nyingi. Kwa haraka pasipo utulivu, tunajidanganya kwa kuamini kwamba tunaweza kumfuata Mungu bila kuacha kila kitu kingine ambacho kinavuta usikivu wetu. Tunapotumia mawazo haya ya uwongo katika kutembea kwetu na Mungu, tunakuwa tumedanganywa.

Kuwa Tayari Kuacha Yaende

Hatuwezi kuwa na kila kitu – hatuwezi kuukumbatia ulimwengu na anasa zake za kimtego na baraka za Mungu. Kufikiri hivyo ni kosa la kufisha. Mtazamo huu wa ununuzi unaambukiza fikra zetu na kuathiri maisha yetu ya kiroho.

10 SIKU ZA MAOMBI

Hatuwezi kuwa na Mungu juu ya kila kitu kingine, kama kuweka kiikizo (icing sugar) kwenye keki, bila kudhamiria kumtengenezea nafasi katika msongamano wa maisha yetu yenye shughuli nyingi. Kwanza ni lazima tuwe tayari kuishi tukiwa na vichache ili kupata baraka za vitu muhimu zaidi. Ni lazima tuache mambo yanayotuvuta kutoka katika uwepo wa Mungu na kuharibu nguvu zetu za kimwili, kiakili, na kiroho. Tunapajaribu kuchanganya ratiba zilizojaa msongamano kwa kasi inayoongezeka kila wakati orodha zetu za mambo ya kufanya zinavyozidi kuwa ndefu na zaidi, tunajikuta kwa haraka tumechoka kimwili na kudhoofika sana kiroho.

Ishi kwa Vichache

Je, mparanganyiko katika maisha yako unakuzuia kuishi kikamilifu kwa ajili ya Mungu? Maisha yenye mlundikano wa vitu vingi humwachia Muumba wa ulimwengu wote nafasi kidogo sana. Lazima tuelewe kuwa na vichache ni bora zaidi. Hatuwezi kupata uzoefu wa baraka zaidi za kiroho, muda zaidi wa maombi, zaidi ya chochote katika maisha yetu ya kiroho ikiwa tu tutajaribu kukiongeza kwenye sahani ilijojaa tayari. Msongamano kama huo huongoza katika utupu zaidi. Badala yake, ni lazima tufanye uamuzi wa kimakusudi kuishi kimakusudi tukiwa na vitu vichache ili tuweze kufurahia zaidi yale yaliyo muhimu kwa Mungu. Kuwa na vichache ni bora zaidi!

Tuombe pamoja.

Muda wa Maombi (Dakika 30 – 45)

Vikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yoyote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nyingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana

10 SIKU ZA MAOMBI

na mada. Unaweza kuomba kupitia vifungu vingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi. Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa mawazo ya maombi.

Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu - Efe. 5:15, 16

“Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenyе hekima; mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu.”

“Basi Angalieni Sana Jinsi Mnavyoenenda; si Kama Watu Wasio na Hekima Bali Kama Watu Wenyе Hekima”

Mungu, katika kukatishwa tamaa kwetu, tunaomba neema na uwekevu Wako. Tumejaza maisha yetu na shughuli nydingi na mahangaiko. Tunahitaji kufanya matengenezo, utakaso, kuweka vipaumbele upya kwa mambo ambayo kwakweli ni ya muhimu. Tufundishe maana ya kuishi na vitu vichache ili tuweze kuzingatia yale muhimu zaidi. Tunatamani kuwa na hekima yenye hekima kutoka juu. Tuongoze, tunaomba, katika jina la Yesu! Amina.

“Tukiukomboa Wakati”

Mpendwa Bwana wetu Yesu, mara zote Wewe huwa unao wakati mwafaka, na Unajua kile kinachopaswa kusemwa na kufanywa kila wakati katika historia. Asante kwa huduma Yako kamilifu kwa ulimwengu huu. Tanaomba utufundishe jinsi tunavyoweza kutumia vyema muda wetu kwa ajili Yako, hasa katika muktadha wa siku za mwisho. Tufunulie pale tunapopoteza muda wetu na utupatie ushindi juu ya mambo tunayojuja yanachukua nafasi kubwa katika maisha yetu. Tanaomba haya katika jina la Yesu! Amina.

“Maana Zamani Hizi ni za Uovu”

Mungu wetu, tunaelewa kwamba ulimwengu unakaribia mwisho. Ishara zinaonekana kila mahali. Hata hivyo, nyakati fulani tunazongwa sana na shughuli zetu, au udanganyifu, kiasi

10 SIKU ZA MAOMBI

kwamba tunasahau kwamba tuko kwenye ukingo wa umilele. Tuongoze katika kujisalimisha kikamili Kwako na huduma uliyo nayo kwa ajili yetu kila mtu binafsi. Rekebisha maisha yetu ili yapatane na mapenzi Yako. Katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo tunaomba! Amina.

Mapendeleko ya Maombi Zaidi

Shukrani na Sifa: Shukuruni kwa baraka mahususi na Mumsifu Mungu kwa wema Wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

Uongozi: Muombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

Mahitaji ya Eneo Mahalia: Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

Sikiliza na Utike: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

Mapendeleko ya Nyimbo

- Jaza Kikombe Changu. No. 287 (VV)
- Kazi Yangu Ikiisha. No. 177. 365 (VV)
- Tafuta Daima Utakatifu. No. 134. 284 (VV)
- Moyoni. No. 211. 400 (VV)

Vipaumbele vya Imani

Siku ya Pili

Hatari ya Kukosa Nafasi kwa Mungu

Fungu Elekezi: *Na mitume wakakusanyika mbele ya Yesu; wakampa habari za mambo yote waliyoyafanya, na mambo yote waliyoyafundisha. Akawaambia, Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo. Kwa sababu walikuwako watu wengi, wakija, wakienda, hata haikuwapo nafasi ya kula. Wakaenda zao faragha mashuani, mahali pasipokuwa na watu.* —Marko 6:30 – 32.

Kujishughulisha katika Kazi kwa Ajili ya Mungu

Kujishughulisha ni jambo la muhimu sana katika dunia yetu. Jamii ya kisasa na shinikizo la juu la matumizi yametuwekea imani moja ndani yetu kwamba: kadiri tunavyojishughulisha sana, ndivyo tunavyoheshimiwa zaidi. Kujishughulisha kumekuwa kiashiria cha bidii na shauku yetu ya kupata mafanikio na kusonga mbele. Lakini tukiwa tunajishughulisha sana *kutafuta riziki*, tumesahau *kuishi* na kufurahia maisha, jambo ambalo ni la kusikitisha. Pengine mbaya zaidi ni hatari mbaya zaidi yani kwamba wafuasi wengi walijitolea wa Kristo wamechukua: mawazo ya kujishughulisha sana katika kazi yao kwa Mungu. Maranyaingi tunafanya hivyo tukiwa na sababu bora zaidi. Tunajua kuwa wakati ni mfupi. Tunataka kutimiza mengi kwa ajili Yake. Kwa hiyo, tunajitahidi kujitumikisha sana. Tunataka kuwa wasimamizi wazuri wa wakati wetu na vipaji. Inapendeza kujishughulisha sana kwa ajili ya Mungu, na wakati mwagine tunajaribiwa kufikiri kwamba Mungu atatuzawadnia tunavyojishughulisha sana kwa ajili Yake, na hatimaye tunagundua kwamba katika kujishughulisha kwetu kwa ajili ya Mungu, tumepeoteza

10 SIKU ZA MAOMBI

muunganiko wetu hai na Mkombozi wetu. Tunafanya mambo mema kwa mazoea, si kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Na kadiri tunavyokuwa tunajishughulisha zaidi, ndivyo tunavyojidhania kuwa tunafanya kwa kupatana na kusudi la Mungu. Kujishughulisha kupindukia kunakuwa kawaida mpya. Tunahangaika kusifia vile tunavyoshughulika sana kiasi kwamba tunakosa nyakati za muhimu sana maishani. Kujishughulisha kupindukia huvunja nguvu zetu za kiroho. Kuwa na haraka ni adui wa uhusiano wowote wa upendo, hasa uhusiano wetu na Mungu aliye hai wa Maandiko. Upendo unahitaji umakini wa wakati usio wa kuharakisha.

Wajibu wa Kupumzika

Haishangazi kuona kwamba Mungu wa Maandiko tena na tena anatuita kusimama tu, kutulia, ili kuona kile atakachowafanyia watu Wake (2 Nya. 20:17; Zaburi 37:7). Mungu anawahimiza watoto Wake kutokuwa na haraka. Anajua jinsi tunavyompoteza upesi wakati akili zetu zimefungwa katika msongamano wa shughuli zetu. Mojawapo ya utambuzi mzuri sana katika hatari ya kujishughulisha sana kwa ajili ya Mungu unapatikana wakati Bwana wetu Yesu alipojitalia uhuru wa kupumzika katika huduma Yake mwenyewe. Ellen White ananasa kwa uzuri kipengele hiki muhimu cha huduma Yake pamoja na wanafunzi Wake: "Walikuwa wakiweka roho zao zote katika kazi kwa ajili ya watu, na hii ilikuwa inachosha nguvu zao za kimwili na kiakili. Ilikuwa ni wajibu wao kupumzika" (*The Desire of Ages*, uk. 360).

Shughuli nyingi zinavunja nguvu na ufanisi wetu wa kiroho. Uharaka ni adui mkubwa wa upendo wetu kwa Mungu. Badala ya kuongeza vitu vingi zaidi kwenye kalenda yetu, hebu na tukusudie kupunguza na kutenga muda tulivu wa kuwa wakati maalum na wenye kuimarisha nafsi pamoja na Muumba na Mwokozi wetu.

10 SIKU ZA MAOMBI

Hebu na tuombe pamoja.

Muda wa Maombi (Dakika 30 – 45)

Vikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yo yote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nydingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana na mada. Unaweza kuomba kupitia vifungu vingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi. Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa matwazo ya maombi.

Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu—Marko 6:30 – 32

“Na mitume wakakusanyika mbele ya Yesu; wakampa habari za mambo yote waliyoyafanya, na mambo yote waliyoyafundisha. Akawaambia, Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo. Kwa sababu walikuwako watu wengi, wakiija, wakienda, hata haikuwapo nafasi ya kula. Wakaenda zao faragha mashuani, mahali pasipokuwa na watu.”

“Njoni Faraghani”

Baba, tumekuwa tukishughulika sana kufanya kazi Yako kiasi kwamba tumesahau kuwa ni kazi Yako. Tunakushukuru kwa kutukumbusha hitaji letu la kuja, na kupumzika, na kuburudishwa. Asante kwa kuwa sisi sio mashine bali wanadamu. Utusamehe tunapofanya shughuli zetu kuwa sanamu au tunapojenga thamani yetu kwa kiasi ambacho tunatimiza kwa ajili Yako. Tafadhali geuza shughuli zetu kuwa uaminifu. Katika jina la Yesu tunaomba; Amina.

“Mahali Pasipokuwa na Watu”

Mungu wetu, tumetumia muda wetu mwangi kwenye kelele nydingi sana, kwa vitu vingi sana, kwa vikwazo vingi sana. Iwe tunatumia muda wetu kufanya kazi kwa ajili ya kanisa au kujishughulisha na

10 SIKU ZA MAOMBI

shughuli nyinginezo, tunatambua hitaji letu la kuacha na kutumia muda kutafakari na kupumzika mbali na shughuli nyingi za maisha. Tafadhalii tupe neema inayohitajika ili tuweze kutenga wakati wa kuwa peke yetu na Wewe kila siku ili kupumzika na kuzingatia kile ambacho ni muhimu sana. Tunaomba haya katika jina la Yesu; Amina.

Mkapumzike Kidogo

Bwana Yesu mpendwa, ulipokuwa ukitembea hapa Duniani, ulielewa hitaji la wanadamu la kupumzika. Asante kwa kuonesha maisha yenye uwiano tunayopaswa kuishi. Tuoneshe jinsi ambavyo mapumziko sahihi yalivyo na jinsi tunavyoweza kupumzika mara kwa mara ili kuongeza nguvu na kuanza upya. Tunaomba haya katika jina la Yesu; Amina.

Mapendekezo ya Maombi Zaidi

Shukrani na Sifa: Shukuruni kwa baraka mahususi na Mumsifu Mungu kwa wema Wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

Uongozi: Muwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

Mahitaji ya Eneo Mahalia: Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

Sikiliza na Utike: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

Mapendekezo ya Nyimbo

- Naja Shambani. No. 297. (VV)
- Karibu na Mungu. No. 276. (VV)
- Huficha Nafsi Yangu. No. 317. (VV)

Vipaumbele vya Imani

Siku ya Tatu

Baraka ya Kusubiri

Fungu Elekezi: *Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu – Zaburi 46:10.*

Sifa ya Kibiblia ya Kutulia

Katika zana za kukimbia huku na kule na uchafuzi wa kelele, hakuna kitu muhimu zaidi kuliko ukimya na utulivu. Katika maisha yetu ya kisasa yenye shughuli nyingi, haraka za kila siku zinahitaji usikivu wetu. Tumezoea kufikiria vyakula vya haraka ambapo tunatarajia mambo kwa njia ya haraka iwezekanavyo. Tumesahau namna ya kungoja kwa subira, na ukosefu huu wa subira unaweza kujulikana katika tembea yetu yamaisha ya kiroho yakiwa na matokeo mabaya. Misukumo ya wazi na sauti za vurugu katika zama hizi miunganiko mingi hufanya iwe vigumu zaidi kupunguza mwendo na kutulia. Kujifunza kusubiri kwa utulivu na kuelekeza mawazo yetu katika mambo ya mbinguni tunapozungumza na Mungu kunaweza kuonekana kuwa jambo geni kwa watu wengi leo, lakini ni maadili ya kibiblia yanayohitaji kuamshwa. Kudumisha mazingira tulivu ambayo hayajasongwa na shughuli nyinginezo na kuhifadhi wakati ulioandaliwa ni muhimu ili kuungana na Mungu. Kupunguza mwendo, kuketi kwa utulivu, kupumua, kujikumbusha juu ya utunzaji mahiri wa Mungu, kungoja kwa subira, na kutokuwa na wasiwasi ikiwa Mungu hatajibu maombi yetu mara moja – hizi ni fani ambazo tunahitaji kujifunza upya.

Faida za Kusubiri

Kote katika Maandiko, tunakutana na watu wa Mungu katika mtazamo wa usikivu wa kusubiri. Waandishi wa Biblia mara nyingi hueleza tarajio lao la kungojea kwa

10 SIKU ZA MAOMBI

swali: "Ee Bwana, hata lini?" (Hab. 1:2; Dan. 8:13). Hakuna tumaini bila kungoja (Tito 2:13). Hakuna saburi bila kungoja (Rum. 5:3, 4). Hakuna subira bila kungoja (Ufu. 14:12). Hakuna tarajio bila kungoja (Zaburi 42:1). Hakuna maisha bila kungoja. Hakuna historia ya mwanadamu bila kungoja. Kusubiri ni sehemu ya uwepo wa mwanadamu.

Tunapongojea, mara nyangi tunakaza macho yetu kwenye shida ambazo hazifurahishi na kutumai kwamba zitapita. Lakinikungojeahaimaanishikukaatubilakufanyachochote, na kutumaini kwamba hali isiyofurahisha itatoweka. Kutoka katika mtazamo wa kibiblia, kusudi la msingi la kungoja ni kudhihirisha Mimi ni nani na Ninakuwa nani ninaposubiri. Uzoefu wa kungoja unanikabili ukiwa na uamuza muhimu wa kiroho: Je, katika kutokuwa na subira na mashaka yangu ninatilia shaka wema wa Mungu na uweza Wake? Au je, ninatambua kwamba katika kungoja, ninapata fursa ya pekee ambayo itanisaidia kuwa mtu ambaye Mungu anataka niwe? Kupitia uzoefu wa kungoja, naweza kuwa mtu ambaye nisingewahi kuwa vinginevyo.

Tukiangalia hili kwa njia hii, kusubiri kunakuwa njia ya Mungu ya kutubadilisha, kutubadilisha kulingana na mapenzi Yake. Kwa hivyo, kungoja ni onesho la kweli la wema na neema ya Mungu. Kunatusaidia kuwa kama Mungu zaidi, ambaye anangoja kwa subira kubwa, bila kutaka ye yote apotee ambaye bado angeweza kuokolewa.

Hebu na tuombe pamoja.

Wakati wa Maombi (Dakika 30 – 45)

Kuomba Sawa na Neno la Mungu – Zaburi 46:10

"Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu."

"**Tulieni**"

Baba Mungu, tumekuwa na wahaka. Tumeruhusu sisi wenyewe kuwa na shughuli nyangi na msongo, tukifikiri kwamba ikiwa hatutafanya hivyo, basi kwa namna fulani hatuna thamani. Ee,

10 SIKU ZA MAOMBI

Mungu tunaomba msaada Wako ili tuweze kutulia, na kujifunza kusubiri tu. Akili zetu zimefungamanishwa na matarajio ya kijamii kila wakati kushughulika kufukuzia kitu fulani. Tusaide kuthamini wema wa utulivu na kupata baraka zinazotokana na kutulia. Tamka maneno "Tulia" ndani ya mioyo yetu isiyo na subira. Tunaomba haya katika jina la Yesu; Amina.

"Mjue ya Kuwa Mimi ni Mungu"

Mpendwa Yesu, ukweli kwamba Wewe ni Mungu na Bwana wetu una maana kubwa katika maisha yetu. Lakini bado tunaonekana kusitasita kukufanya Wewe kuwa Bwana wa maisha yetu yote. Tunatamani utawale, na hatuonekani kuweza kuacha kufanya kile tunachofanya. Utufundishe kwamba Wewe, Muumba Mwenyezi, Udimuaye milele, ndiwe Bwana; kwamba Unaweza kutuchukua sisi na mipango yetu zaidi ya kitu chochote tunachoweza kufikiria ikiwa tu tutatulia, kusubiri, na kukutambua Wewe kama ulivyo. Tunaomba haya kwa jina Lako; Amina.

Mapendeleko ya Maombi Zaidi

Shukrani na Sifa: Shukuruni kwa baraka mahususi na Mumsifu Mungu kwa wema Wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

Uongozi: Muombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenyе mahitaji).

Mahitaji ya Eneo Mahalia: Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

Sikiliza na Uitike: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

Mapendeleko ya Nyimbo

- Mapenzi Yako Yafanyike. No. 333 (VV)
- Furaha Gani. No. 43. 251 (VV)

Vipaumbele vya Imani

Siku ya Nne

Uhuru wa Kuchagua Maisha Rahisi

Fungu Elekezi: “Tena mfungapo, msiwe kama wanafiki wenyewe uso wa kukunjamana; maana hujiumbua nyuso zao, ili waonekane na watu kuwa wanafunga. Amin, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso; ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi.” – Mathayo 6:16 – 18.

Kufunga Hutengeneza Nafasi

Njia moja ya kutengeneza nafasi ya kuishi maisha ya kumwelekea Mungu ni kufunga. Kufunga maana yake ni kutenganisha akili na maisha yetu kwa makusudi kabisa kutoa nafasi kwa ajili ya kuongozwa na Roho Mtakatifu ndani yetu na kwa kumzingatia Mungu na Neno Lake. Biblia mara kwa mara hutaja kufunga katika mwunganiko na maombi. Yesu alifunga kabla hajaanza huduma Yake ya hadhara (Mt. 4:2; Lk. 4:2). Mitume walifunga na kuomba ili kuongozwa na Mungu (Mdo. 13:2, 3), na katika Agano la Kale kufunga kulifanywa mara kwa mara mionganoni mwa wanaume na wanawake walioamini (1 Wafalme 21:9, 12; 2 Nya. 20:3; Ezra 8:21; Esta 4:3, 16; Isa. 58:6; Yer. 36:9; Dan. 9:3; Yoeli 2:12; Yoh. 3:5; n.k.).

Tofauti na kufunga kwa afya njema, kufunga katika Biblia sio kuzingatia lishe maalum iliyoundwa kwa ajili ya kupunguza uzito na ustawi. Badala yake, ni uamuza wa kukusudia kujiepusha na chakula na shughuli za bughudha kwa muda ili kuomba na kuzungumza na Mungu. Kwa kuacha kwa muda tuliyozoea, tunapata uhuru mpya wa kiroho. Wakati wa kufunga na kuomba, lengo la maisha ya kila siku hubadilika: mbali na kutosheleza mahitaji

10 SIKU ZA MAOMBI

yetu wenyewe, mbali na kazi zetu wenyewe, na tunakuwa na utii katika kumsikiliza Mungu. Kufunga kwa Kibiblia kunaonesha shauku yetu ya kuongeza utegemezi wetu kwa Mungu na kuzingatia mambo ya kiroho ambayo ni muhimu. Hii inajumuisha zaidi ya kutokula; kwa kweli, hili linatia changamoto katika kila eneo la maisha yetu. Katika kufunga, tunakubali kwamba tunataka kutoa nafasi kwa ajili ya Mungu kwa kupunguza vikwazo vyovyyote vinavyozonga usikivu na shauku yetu. Tunaonesha kwamba tunataka kutafuta na kuthamini uwepo wa Mungu katika maisha yetu kuliko kitu kingine chochote.

Kujinyima na Kujumuisha

Je, tunawezaje kuishi maisha haya ya usahili, ambapo tunajifunza kuzingatia mambo ambayo kweli ni muhimu? Kama vile tunavyohitaji kuwa makini kwa kile tunachokula, lazima tuzingatie kile tunachotazama na kile kinachoingia masikioni mwetu. Tunachosikiliza huathiri mawazo yetu sawa na vile tunavyoona. Ni aina gani za muziki, vitabu, podikasti, au tovuti ambavyo huzalisha mawazo yenye sumu au kwa ubatili kuchukua muda wako wa thamani? Mbali na kujiepusha na mambo fulani, huenda ukahitaji kujumuisha kwa makusudi tabia mpya ili kukusaidia kujenga na kuunda mawazo yenye afya na ya uponyaji.

Usahili wa Maisha, akili isiyo na mkanganyiko, haitokani na yale ambayo ulimwengu unatuambia tutafute. Moyo wa kuridhika huja kwa kumwamini Mungu. Tunapojifunza kumtazama Yeye, badala ya kile ambacho wengine wanafanya, na tunapojizoeza kuacha mambo yanayotukengeusha, tunagundua maisha rahisi ya pumziko na amani pamoja na Muumba na Mkombozi wetu.

Hebu Tuombe pamoja.

Wakati wa Maombi (30 – 45)

Kuomba Kulingana na Neno la Mungu – Mathayo 6:16 – 18.

"Tena mfungapo, msiwe kama wanafiki wenyе uso wa kukunjamana; maana hujumbua nyuso zao, ili waonekane na watu kuwa wanafunga. Amin, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso; ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi."

"Tena Mfungapo"

Baba yetu wa Mbinguni mwenye upendo, asante kwa kutupatia chochole tunachohitaji. Katika ziada na wingi wetu, mara nyingi tunasahau kwamba kitu kikubwa kupindukia sio kizuri kamwe. Bwana, kufunga hakuji kwa kawaida, na kwa hivyo tunakusihii utupatie nguvu ya kuchagua kujiepusha na anasa na kujiepusha na kitu chochole kibaya, iwe ni chakula, muziki, sinema, manunuzi, n.k. Pia, tuoneshe jinsi tunavyoweza kukusudia zaidi katika kubadilisha kisicho na faida na kilicho na faida. Tusaidie kuchagua mtindo wa maisha kamili, wenyе afya. Tunaomba haya katika jina la Yesu; Amina.

"Kama Wanafiki"

Ee Mungu, tunatamani badiliko la moyo. Tunaomba utusamehe kwa unafiki wetu, kwa kuwa kila tunaposema, tunapofundisha, au tunapohubiri kitu hiki, sisi tunaishi kitu kingine. Tunataka kufanya mambo tunayokufanyia kutoka katika moyo uliokabidhiwa Kwako, moyo unaosukumwa na upendo, moyo unaofanywa upya kwa rehema na neema Yako na uwepo wa kudumu wa Roho Mtakatifu. Tunaomba kufunga kwetu, na shughuli zetu zote za kiroho na za kila siku, ziwe onesho la kweli la uwepo Wako mtakatifu ndani ya miyo yetu. Tunaomba haya katika jina la Yesu; Amina.

10 SIKU ZA MAOMBI

Mapendekezo Zaidi ya Maombi

Shukrani na Sifa: Shukuruni kwa baraka mahususi na Mumsifu Mungu kwa wema Wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

Uongozi: Muombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

Mahitaji ya Eneo Mahalia: Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

Sikiliza na Uitike: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

Mapendekezo ya Nyimbo

- Yote Namtolea Yesu. No. 122, 332 (VV)
- Namtaka Bwana Yesu. No. 145, 155 (VV)

Vipaumbele vya Imani

Siku ya Tano

Kulenga Mambo Muhimu katika Maombi Yetu

Fungu Elekezi: “Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.” – Mathayo 6:9, 10

Mtizamo Mpya katika Maombi

Kumtazama Mungu na katika mambo ya muhimu ni muhimu katika maisha yetu ya maombi vile vile. Mara nyingi maombi yetu ni dhaifu na yasiyo na nguvu kwa sababu yanatuhusu sisi wenyewe tu. Tunamwomba Mungu yale tunayotamani kuwa nayo. Tunazingatia mahitaji yetu na changamoto tunazokabiliana nazo badala ya kumtazama Mungu.

Maombi yanayompendeza Mungu yana mtazamo tofauti uhuishao. Jambo kuu sio “orodha ya vitu tutakavyo” tena, bali ni Mungu Mwenyewe. Mtazamo huu ndio ufunguo wa uzoefu mpya wa maombi. Maombi yanayompendeza Mungu kwanza yanamtambua Mungu kuwa rafiki yangu mwaminifu ambaye ninatafuta kuwa na uhusiano Naye wa kina kwa sababu Yeye ni muhimu kwangu, si kwa sababu ninataka kitu kutoka Kwake. Yeye Mwenyewe, ni muhimu zaidi kuliko vitu anavyonipa. Kumjua Yeye ndiyo sababu ninataka kuzungumza Naye kabisa. Bila Yeye, maisha yangu hayana msingi na hayana mtazamo unaofaa. Muhimu zaidi kuliko chochote ninachoweza kuomba kinapasa kiwe shauku yangu ya kuwa pamoja Naye. Uwepo Wake na Yeye Mwenyewe huwa kitovu cha maombi ya kweli.

Maombi Ambayo Mungu Ndiye Kiini Hubadilisha

Maombi ambayo yanampendeza Mungu yanaanza na shauku ya kuwa pamoja Naye. Hayaanzi na matakwa na mahitaji yangu. Wakati maombi yangu hayajatia nanga

10 SIKU ZA MAOMBI

katika uhusiano huu wa upendo na Yeye, yanahusiana na matakwa yangu zaidi kuliko kwa Mungu na mapenzi Yake. Mara ninapoelewa kuwa uhusiano wangu na Mungu ndio kitovu cha maombi, maombi yangu hupata mwelekeo mpya kabisa. Ninaanza kufikiri na kuomba kutoka katika mtazamo wa Mungu. Ninaanza kufikiria na kuomba kutoka kwa mtazamo wa Mungu. Ninaanza kutazama maombi yangu, matakwa yangu, matamanio yangu, na maisha yangu yote kupitia macho Yake. Mtazamo huu unafanya maombi kuwa ya maana. Ondoa kipengele cha uhusiano kutoka kwenye maombi, na kisha maombi yanakuwa ya upande mmoja, ya ubinaksi na mbaya. Maombi yanayomhusu Mungu huweka huru mawazo yangu dhidi ya kujifikiria nafsi. Hunisaidia kuwa mkweli kwa Mungu.

Katika nuru ya upendo na utakatifu Wake, ninaanza kujiona wa tofauti. Kusudi la kweli la maombi sio utimizwaji wa matakwa yangu lakini ni kuimarisha uhusiano wangu na Mungu anayebadilisha maisha. Ni rahisi sana kumwomba Mungu kitu kabla sijafurahia ushirika Wake.

Ninapofikiria kwa uangalifu tabia ya Mungu, sifa Zake, na kile Anachowenza kufanya, na ninapodhihirisha upendo kwa maneno yangu mwenyewe, sala zangu hujawa na maisha ya kiroho, upendo, na kicho. Maombi yangu hayahusiani tena na matatizo yangu bali Mungu, ambaye ndiye Bwana wa mahitaji yangu yote. Maombi kama haya huniinua mbele Zake. Hayambadilishi Mungu; yananibadilisha. Kwa nini usianze kuomba hivyo? Itabdalilisha maisha yako.

Hebu tuombe pamoja.

Wakati wa Maombi (30 – 45)

Kuomba Kulingana na Neno la Mungu – Mathayo 6:9, 10.

“Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.”

10 SIKU ZA MAOMBI

"Baba Yetu Uliye Mbinguni, Jina Lako Litukuzwe"

Baba yetu Mwema wa Mbinguni, Wewe ndiwe Mungu. Wewe ni muweza, Mwenye kujua yote, wa ajabu, na Uliye mkuu. Wewe ni mwema na wa ajabu. Wewe ni Kweli, Haki, na Upendo. Tunatamani kukujua Wewe zaidi sana. Tunataka kuthamini kila siku tabia Yako, uweza Wako, tukujue Wewe, na mapenzi Yako. Tunaomba utukomboe kutoka katika mtazamo wetu wa ubinafsi, na yafanye maombi yetu yawe yanakukutanguliza Wewe. Katika jina la Yesu tunaomba; Amina.

"Ufalme Wako Uje, Mapenzi Yako Yatimizwe"

Bwana, ufalme wako ndio chombo pekee cha kiserikali tunachotaka kuweka kiapo cha utiifu wetu kwake. Utawala Wako ni wa upendo, kweli, haki na wa uadilifu. Mawazo, mipango, na mbinu zetu si kamilifu, lakini mapenzi Yako daima ni makamilifu. Tunaomba ufalme wako uenee katika mioyo na maisha yetu leo. Tunaomba utujulishe Wewe Ulivyo. Katika jina la Yesu tunaomba; Amina.

Mapendekezo Zaidi ya Maombi

Shukrani na Sifa: Shukurani kwa baraka mahususi na Mumsifu Mungu kwa wema Wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

Uongozi: Muombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

Mahitaji ya Eneo Mahalia: Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

10 SIKU ZA MAOMBI

Sikiliza na Utike: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

Mapendekezo ya Nyimbo

- Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu. No. 1, 23 (VV)
- Saa Heri ya Maombi. No. 135, 278 (VV)
- Bwana Mungu. No. 28 (VV)

Vipaumbele vya Imani

Siku ya Sita

Ujasiri, Shauku Kali na Uvumilivu

Fungu Elekezi: “*Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.*” – Wagalatia 6:9.

Ujasiri wa Kiroho

Ujasiri ni kitu ambacho mara kwa mara hatukihusishi na mambo ya kiroho. Lakini ni muhimu katika harakati zetu za kila siku za kuutafuta utakatifu kama ilivyo katika maeneo mengine ya maisha, kutoka kwa michezo hadi katika kujifunza shughuli za biashara zenyе mafanikio. Bila ujasiri, mafanikio hayawezekani. Ujasiri ni shauku kali na uvumilivu wa kufukuzia lengo tunalolijali sana. Ili kuweza kufikia malengo yetu, tunayapangilia maisha yetu kwa namna ambayo hakuna kitu kitakachotuzuia. Tunahitaji ujasiri wa namna hii katika kutembea kwetu kiroho na Mungu, na tunauhitaji kwa namna ya pekee katika maisha yetu ya maombi. Mara nydingi, hatuoni matokeo ya maombi yetu kwa sababu hatuombi pasipo kukata tamaa katika maombi yetu. Huenda tunazuiwa au kuvunjwa moyo, au tunakata tamaa mioyoni mwetu hatuamini kwamba Mungu anaweza kusikia na kutenda kwa njia ambayo hupita uelewa wetu. Katika Luka sura ya 18, Yesu anawahadithia wanafunzi Wake kisa cha mwanamke mjane ambaye alidumu kuleta kesi yake kwa hakimu dhalimu. Ingawa hakimu huyo hakumjali Mungu wala mwanamke huyo, hatimaye alikubali ombi la mjane huyo kwa sababu ya kuendelea kwake (Luka 18:1 – 7).

Mungu, hata hivyo, sio kama alivyokuwa yule hakimu dhalimu asiyejali maombi yetu. Mungu ana shauku ya kutusaidia zaidi ya vile tunavyoweza kuelewa (Yer. 33:3).

10 SIKU ZA MAOMBI

Kile tunachokihitaji leo, katika ndoa zetu, katika madarasa na mabweni yetu, kanisani na nyumbani kwetu, ni watu wanaoomba. Sio tu wale wanaozungumzia maombi, wale wanaosema wanaamini katika maombi, au hata wale wanaoweza kutoa maelezo mazuri kuhusiana na maombi. Kwa hakika tunahitaji watu wanaotumia kila fursa ili kuomba!

Ung'ang'anifu

Mungu hafanyii kazi maneno ya haraka na rahisi. Mara nyingi katika pambano kuu kati ya Mungu na Shetani tunahitaji maombi ya kung'ang'ania. Ni lazima tuwe na uhitaji mkuu na kung'ang'ana katika maombi yetu kwa sababu ratiba za Mungu mara nyingi hazilandani na ufahamu wetu wa kibinadamu. Mungu hachukui njia rahisi anaposhughulika katika kufanya kazi zitakazo majibu ya kimbingu. Hapendezwi na njia rahisi bali huchagua njia bora zaidi! Katika maombi yetu, hebu tusiridhike na mambo machache au kubaki tukiwa tumeridhishwa na malengo yasiyoona mbali. Mungu anafurahia tunapong'ang'ana katika maombi yetu.

Katika chumba cha kujisomea cha baba yangu, ambaye alikuwa mwinjilisti na mchungaji mwenye mafanikio, alikuwa na nukuu kutoka kwa Ellen G. White ambayo iliacha mguso wa kina ndani yangu: "Ushindi mkubwa zaidi kwa kanisa la Kristo au kwa Mkristo binafsi sio ule unaopatikana kwa talanta au elimu, kwa mali au upendeleo wa wanadamu. Ni ule ushindi unaopatikana katika chumba cha mazungumzo pamoja na Mungu, wakati imani yenye bidii, yenye uchungu inaposhikilia mkono wa Mungu wenye uweza" (Patriarchs and Prophets, uk. 203, *msisitizo umewekwa*).

Hebu tuombe pamoja.

10 SIKU ZA MAOMBI

Wakati wa Maombi (30 – 45)

Kuomba Kulingana na Neno la Mungu – Gal. 6:9

“Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.”

“Tena Tusichoke Katika Kutenda Mema”

Bwana Yesu, Wewe ndiye Kiumbe pekee mvumilivu zaidi ulimwenguni. Hukukata tamaa katika huduma Yako ya maombezi nakuilingilia kati. Haijalishi Shetani na wenyе dhambi wanakutupia nini, Wewe bado ni Wewe, na katika upendo, Unajitoa kwa ajili yetu. Tunaogopa, ee Mungu. Tunaomba utufundishe uvumilivu kama huo wa kiroho, usio na ubinafsi, haswa katika maisha yetu ya maombi. Utufanye mashujaa wa maombi wasiokata tamaa. Tunaomba haya katika jina la Yesu; Amina.

“Tutavuna kwa Wakati Wake”

Mungu wetu mwenye upendo, tunakusifu kwa kuturuhusu kushiriki katika utume Wako katika sayari hii. Asante kwa furaha ya huduma na furaha ya kushiriki katika kazi ya kuwaleta watu Kwako. Wakati fulani tunajisikia kuvunjika moyo na kuwa tayari kukata tamaa, lakini tunaomba kwamba utupe uvumilivu na ujasiri wa kiroho unaohitajika ili kufanya kazi uliyotuita kuifanya. Asante kwa kuwa Unapenda kutubariki na kwamba tutaona matunda ya huduma hii iliyobarikiwa. Tunaomba haya katika jina la Yesu; Amina.

Mapendekezo Zaidi ya Maombi

Shukrani na Sifa: Shukuruni kwa baraka mahususi na Mumsifu Mungu kwa wema Wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

Uongozi: Muombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

10 SIKU ZA MAOMBI

Kanisa Letu: Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

Mahitaji ya Eneo Mahalia: Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

Sikiliza na Utike: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

Mapendekezo ya Nyimbo

- Fanyeni Kazi zenu. No. 59, 205 (VV)
- Taamini Nitii Pia. No. 336 (VV)
- Nakaza Mwendo Mbinguni. No. 73

Vipaumbele vya Imani

Siku ya Saba Thamani ya Kuwa Mwema

Fungu Elekezi: “*Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.*” — Yohana 13:35.

Sifa Inayokutambulisha

Mwishoni mwa maisha yako, ikiwa ungekumbukwa kwa sifa moja tu ya kitabia, je, ingekuwa sifa gani? Ikiwa sifa moja tu ingeonesha kile ulichosimamia na ulichothamini zaidi, ungechagua nini? Majibu mengi yanaweza kutolewa, lakini kipengele kimoja muhimu cha tabia ya Mungu kinapaswa kuoneshwa katika maisha yetu yote. Katika Tito 3:4, Biblia inatuambia kwamba wema wa Mungu, Mwokozi wetu, ulionekana kwetu wakati upendo Wake ulipotuokoa.

Wema! Wema wa Mungu. Wema ni lugha ya ulimwenguni pote inayoweza kueleweka na wazee na vijana, matajiri na maskini, wanaume na wanawake, viziwi au vipofu. Wema hauna kizuizi cha lugha. Una mvuto wa ulimwengu wote, kama muziki. Tabasamu la kirafiki, mkono wa usaidizi wakati wa mahitaji, msaada tunapohisi kuvunjika moyo, na neno la kutia moyo — yote yanasaidia sana kufanya ugumu wa maisha yetu kuwa rahisi na kuvumilika zaidi. Wema haukugharimu sana, lakini unaweza kuleta mabadiliko makubwa katika maisha ya wale wanaoupokea, kadhalika katika maisha ya wale wanaoushiriki na wengine. Wema ni kwa ajili ya wote mtenda na mtendewa.

Mkristo Mwema

Bwana Yesu alijua kwamba wema wa wafuasi Wake ungetumika kama ushuhuda mkubwa sana wa imani yao. Punde tu baada ya kusalitiwa na kifo Chake, baada ya kuwanawisha miguu wanafunzi Wake, Yesu aliwaambia,

10 SIKU ZA MAOMBI

"Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi" (Yohana 13:35). Ellen White anaitikia utambuzi huu: "Hoja yenyeye nguvu kwa ajili ya injili ni Mkristo mwenye upendo na aliye mwema" (*The Ministry of Healing*, uk. 470). Tunaposhughulika na wengine kwa wema, upendo wetu unaweza kufikia mioyo kwa njia ya pekee nje ya mipaka ya kidini, kikabila na hadhi ya kijamii. Ninaamini kwamba Mungu alituumba tukiwa na shauku ya kupokea na kuonesha wema kwa wengine, na kufanya hivyo kunaonesha tabia ya Mungu tunayemwabudu. Katika Yona 4:2 tunasoma kwamba Mungu ni Mwenye neema na huruma, si mwepesi wa hasira, na mwingi wa rehema. Mada ya rehema za Mungu inaenea katika Biblia yote, Agano la Kale na Jipy.

Matendo yetu ya wema huleta faraja na furaha sio tu kwa wanadamu bali pia kwenye moyo wa Mungu. Wema haukazi macho katika hali mbaya zinazotuzunguka au kwa watu wengine. Badala yake, unaakisi tabia ya Mungu na namna Anavyoshughulika nasi. Hebu natuzingatie mambo muhimu maishani na tufahamike kuwa watu walio wema kwa wote.

Hebu tuombe pamoja.

Wakati wa Maombi (30 – 45)

Kuomba Kulingana na Neno la Mungu – Yohana 13:35

"Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi."

"Hivyo Watu Wote Watatambua ya Kuwa Ninyi Mmekuwa Wanafunzi Wangu"

Baba Mungu, ni mara ngapi utume wetu umekosa uwiano? Tunafanya theolojia, unabii, imani za msingi, mtindo wa maisha, n.k. kuwa lengo kuu. Na ingawa mambo haya ni mazuri, ya kweli, muhimu, na yana jukumu muhimu

10 SIKU ZA MAOMBI

na mahali, Ulihubiri waziwazi na, muhimu zaidi, uliishi ukweli kwamba upendo ndio ufunuo wenyewe nguvu zaidi wa ukweli. Tusaidie kuuishi upendo na wema pamoja na ukweli, kama ulivyouishi milele. Amina.

“Mkiwa na Upendo Ninyi kwa Ninyi”

Bwana Yesu mpendwa, tunaomba utusamehe kwa kukosa upendo usio na ubinafsi. Kwa kweli hatujaufahamu upendo wa Kalwari. Tunaomba utusamehe kwa namna tunavyofikiri juu ya kila mmoja wetu, kile tunachosema kuhusu kila mmoja wetu, na jinsi tunavyotendeana. Tunaomba Bwana, utujaze kwa upendo Wako wa mbinguni. Tunaomba utufanye kuwa mabalozi wa upendo na wema. Watu wamwone Yesu ndani yetu na kwa jinsi tunavyotendeana. Tupatie tunda la Roho katika maisha yetu, tunaomba katika jina la Yesu; Amina.

Mapendeleko Zaidi ya Maombi

Shukrani na Sifa: Shukuruni kwa baraka mahususi na Mumsifu Mungu kwa wema Wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

Uongozi: Muombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

Mahitaji ya Eneo Mahalia: Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

Sikiliza na Utike: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

Mapendeleko ya Nyimbo

- Nataka Nimjue Yesu. No. 54, 98 (VV)
- Nipo Bwana Nitume. No. 107, 210 (VV)

Vipaumbele vya Imani
Somo la Nane
Kuwa na Shukrani

Fungu Elekezi: “Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho.” – Waebrania 12:28.

Mtazamo wa Ukubali

Kuna mtazamo ambao ni muhimu sana kwa Mungu. Katika Biblia, tunahimizwa mara kwa mara kuzoea tabia hii kwa sababu inampendeza Mungu na ni baraka kwetu. Mtazamo huu ni shukrani. Kitabu cha Waebrania kinasema, “Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho” (Waebrania 12:28). Shukurani humpendeza Mungu na huathiri vyema maisha yetu wenyewe kwa sababu hutusaidia kuzingatia kile ambacho ni chanya. Kama msuli, huimarika unapoutumia kimkakati kwa kutambua baraka zako.

Mungu anawaalika watoto Wake kuwa watu wa kushukuru. Katika 1 Thes. 5:18, mtume Paulo anaandika, “shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.” Kutoa shukurani kunamaanisha kukumbuka kwamba mtu fulani amefanya jambo jema kwa ajili yetu na kuonesha shukurani hiyo kwa maneno ya kushukuru. Kukuza mtazamo wa shukurani hufungua macho yetu ili kusikia maelezo mazuri katika asili na kwa watu wengine. Shukrani hutufanya kuwa wenyekushukuru kwa baraka sahili pasipo kudai kuwa wakamilifu. Hii ni muhimu kwa sababu, kwa upande huu wa umilele, maisha kamwe hayataenda vizuri kabisa. Lakini maisha sio lazima yawe kamili ili kufurahiwa! Uzuri hukutana na kuonekana kwa njia nydingi. Harufu nzuri ya ua, uzuri wa anga lenye nyota usiku usio na mawingu, kumeta-meta kwa upendo machoni pa rafiki – kila moja hutukumbusha uzuri ambao Mungu ameuandaan kwa ajili ya wale wanaompenda.

10 SIKU ZA MAOMBI

Hamisho la Usikivu Wetu

Kwa kuonesha shukrani, tunahamisha mawazo yetu kutoka kwenye mambo ya kufikirika tusiyo nayo hadi kwenye baraka halisi tunazofurahia. Shukrani hukua kutohana na utambuzi wa ukarimu wa Mungu na inahusisha shauku ya kuchunguza njia mahususi ambazo kwazo Anaonesha upendo Wake kwetu. Shukrani hizo huongeza upeo wa maisha na huongeza uwezo wetu wa kupata raha na kuridhika.

Tafiti za hivi karibuni zimeonesha kwamba kushukuru sio tu kunaimarisha ustawi wa aitoaye na aipokeaye lakini inaweza pia kuwa njema kwa wale wanaishuhudia. Kushuhudia tendo la shukurani kati ya watu wawili kunaweza kuwafanya watazamaji kujisikia kuwa wachangamfu na mshikamano zaidi kwa hao wote wawili, kulingana na makala ya hivi karibuni ya New York Times . Kwa nini tusifanyie kazi kile ambacho Mungu ametuita ili kukifanya: tukikuza mtazamo wa kushukuru ambao utabadilisha mikutano yetu na watu wanaotuzunguka kuwa bora na kuifanya dunia kuwa ya kupendeza zaidi. Mshukuru Mungu kwa zawadi ya shukurani.

Hebu tuombe pamoja.

Wakati wa Maombi (30 – 45)

Kuomba Kulingga na Neno la Mungu – Ebr. 12:28

“Basikwakuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho.”

“Hebu Tuoneshe Shukurani”

Mungu wetu mwenvye upendo, tunatatizika sana linapokuja suala la kukurudishia kiasi kinachofaa cha shukrani kwa yote Uliyotufanyia. Umilele hautoshi kukupa shukrani unayostahili. Hata hivyo, tunakuomba ufurahie shukrani zetu. Pia tunakuomba utusaidie kuweka kando dharau, hali ya kuhukumu, na kiburi, ili tuweze kutambua baraka ambazo tunaweza kuziona na

10 SIKU ZA MAOMBI

kushukuru. Tusaidie kutumia muda ili kutoa shukrani Kwako na kwa wengine zaidi ya tunavyotoa malalamiko na maombi yetu. Tunakuomba ukuze ndani yetu tabia ya kweli ya shukrani katika jina la Yesu; Amina.

“Kwa Kuwa Tunapokea Ufalme Usioweza Kutikiswa”

Bwana, Wewe ni Mungu mkarimu. Sio tu kwa kutupatia wokovu kwa gharama ya milele Kwako bali pia kwa kutupatia ufalme Wako. Hatutambui ukubwa wa fursa Unazotupatia. Tunaomba utuoneshe kila siku vile ilivyo heshima kubwa kuwa watoto Wako. Asante kwa upendo huu mkubwa na baraka. Tunaomba haya katika jina la Yesu; Amina.

Mapendekezo Zaidi ya Maombi

Shukrani na Sifa: Shukuruni kwa baraka mahususi na Mumsifu Mungu kwa wema Wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

Uongozi: Muombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenyeye mahitaji).

Mahitaji ya Eneo Mahalia: Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

Sikiliza na Utike: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

Mapendekezo ya Nyimbo

- Heshima na Utukufu. No 5 (VV)
- Na Tumwabudu. No. 5, 27 (VV)
- Nasifu Shani ya Mungu. No. 38, 26 (VV)

Vipaumbele vya Imani

Siku ya Tisa

Mbaraka wa Sabato

Fungu Elekezi: “Kama ukigeuza mguu wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenyeheshima; ukiitokuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapo jifurahisha katika Bwana; nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo.” – Isaya 58:13, 14.

Ishara ya Utambulisho Wetu

Mbaraka mmoja wa muhimu kweli kweli kwa manufaa ya wanadamu ni pumziko la Sabato. Siku ya Sabato inatukumbusha kuhusu asili yetu na kwamba Mungu ni Muumbaji wetu (Kut. 20:8 - 11). Pia inashuhudia neema ya Mungu kuwa ni Mwokozi mwenye upendo ambaye aliwakomboawatu Wake kutoka katika kifungo cha utumwa (Kum. 5:12 - 15). Kwa sababu hiyo, raha ya Sabato ni ishara yenyenuguvu ya utambulisho wetu kama wanadamu. Utambulisho huu hautokani na mafanikio ya kiuchumi au kiwango chetu cha uzalishaji. Wala utambulisho wetu hauamuliwi iwapo sisi ni waajiri au waajiriwa. Sabato ni mwaliko wa Mungu kupumzika ndani Yake na kufurahia kile ambacho ametoa kwa neema Yake.

Sabato, ikieleweka vyema, ni uzoefu wa kutulia pasipo haraka. Inatufundisha kupumzika kutoka katika kukimbia huku na kule, katika kushughulika, kutafuta faida. Ni tamko la kila juma kwa moyo na akili yangu kwamba Mungu ni muhimu zaidi kuliko orodha yangu ya mambo ya kufanya na uzalishaji wangu. Inathibitisha mabadiliko katika vipaumbele vyangu na kufanya uaminifu wangu uonekane. Sabato inaniruhusu kupunguza mwendo

10 SIKU ZA MAOMBI

na kupumzika katika uwepo wa Mungu. Inaniruhusu kufurahia ahadi Yake kwamba Yeye anatosha. Ingawa kutojihusisha na shughuli za biashara za dunia hii siku ya Sabato ni onesho muhimu a uaminifu wetu kwa Mungu, kupumzika katika upendo na utunzaji wa Mungu ni zaidi ya kuacha kufanya kazi. Pumziko la Sabato linatimizwa katika ushirika wetu wa makusudi na wenyewe maana pamoja na Muumba wetu. Tunapojoifunza kutulia katika uhalisi wa upendo wa Mungu usioshindwa, na wakati wema Wake unapokuwa lengo letu, tunapata furaha, amani, na shauku ya kumwabudu Mungu kwa nafsi yetu yote.

Kwa hivyo, utunzaji wa Sabato kwa furaha na uaminifu unakuwa ishara muhimu ya sisi ni nani na tu watu wa nani. Ili kufurahia hali ya kiroho ya Sabato tukiwa na nyakati za amani, shangwe, na utulivu huhitaji mengi zaidi ya kujiepusha na kazi siku ya saba. Inahuisha upangaji wa hadhari unaotuandaa wakati wa juma kwa ajili ya mambo makuu ya amani ya Sabato. Kwa hivyo, Sabato inatengeneza hali yenye maana kinyume utamaduni ambao unaonekana katika mtindo tofauti wa maisha. Sabato inatulinda dhidi ya utawala wa uharibifu. Badala ya kuhangaika ili kupata zaidi na zaidi katika mbio zisizo na mwisho za mamlaka na umiliki, tunaalikwa kutulia na kumheshimu Mungu na wema na neema Yake. Hii ni tofauti kabisa na kiburi na ubinafsi wetu. Kwa kuitunza Sabato, tunakuwa wanafunzi wa Yesu Kristo, ambaye aliitunza Sabato kama ilivyokuwa desturi Yake (Luka 4:16).

Kuitakasa Sabato, kuiweka wakfu, na kuiweka maalum kwa Mungu kwa ajili ya kusudi Lake la pekee hutusaidia kukaza fikira zetu kwa mambo ya maana sana katika kutembea kwetu kiroho pamoja na Yesu. Sabato sio siku ya kulala na kutofanya lo lote; badala yake, ni siku ya kumwabudu Mungu wa pekee wa kweli na hivyo inakuwa ishara ya maana kwamba tumeelekeza maisha yetu kwa Mungu aliye hai wa Maandiko.

10 SIKU ZA MAOMBI

Hebu tuombe pamoja.

Wakati wa Maombi (30 – 45)

Kuomba Kulingana na Neno la Mungu – Isaya 58:13, 14

“Kama ukigeuza mguu wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenyeheshima; ukiitokuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika Bwana; nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo.”

“Ukiita Sabato Siku ya Furaha”

Baba yetu, umetupatia zawadi ya pekee sana katika Sabato. Tunakushukuru kwakuwa hukutupatia maisha ya kushughulika kwa saa 24/7 bali kwamba Ultiuumba ili tufurahie ushirika, uwiano na amani pamoja na Wewe kwa namna ya pekee kila siku ya saba. Baba Mungu, mara nyangi sana, tumeifanya Sabato kuwa siku ya shughuli nyangi zaidi ya juma na tumepoteza lengo lake. Utusamehe tafadhali. Tunaomba utufundishe jinsi ya kuitunza na kuitakasa Sabato na kuifanya kuwa ya furaha kwa wote katika nyanja ya mvuto wetu. Tunaomba haya katika jina la Yesu; Amina.

“Wala Kusema Maneno Yako Mwenyewe”

Bwana Yesu, tunakupa heshima na utukufu, kwa maana Wewe ni mtakatifu na Ustahiliye heshima. Asante kwa kuwa Sabato ni siku ambayo tunawekwa huru ili kukutazama Wewe, Neno Lako, Uumbaji Wako, na kuwa baraka kwa wengine. Hata hivyo, mara nyangi sana, tumetumia saa hizi takatifu zilizojaa mazungumzo ya bure na shughuli ambazo hazikuletei Wewe heshima. Tafadhali tusamehe. Tunaomba utufundishe jinsi ya kuifanya Sabato iwe ya kuhuishaa, nzuri, na takatifu. Tunaomba haya katika jina la Yesu; Amina.

10 SIKU ZA MAOMBI

Mapendeleko Zaidi ya Maombi

Shukrani na Sifa: Shukuruni kwa baraka mahususi na Mumsifu Mungu kwa wema Wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

Uongozi: Muombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

Mahitaji ya Eneo Mahalia: Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

Sikiliza na Utike: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

Mapendeleko ya Nyimbo

- Magharibi Jua. No. 92, 18 (VV)
- Ni Siku ya Furaha. No. 82, 214 (VV)
- Tukimngojea. No. 174, 347 (VV)

Vipaumbele vya Imani

Siku ya Kumi

Ujazwe na Vitu vya Muhimu – Kuwa Kianalojia Zaidi

Fungu Elekezi: “Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia.” – Ebr. 10:24, 25.

Analojia ya Kiroho

Hali ya kiroho ya Kibiblia ni ya analogia, sio ya kidijitali. Ina msingi wake katika mazoea binafsi na yaliyo dhahiri kati ya watu halisi na Mungu aliye hai. Vitu halisi katika asili yake ni vya analogia, sio visivyyoshikika. Japokuwa Mungu wa Biblia haonekani kwa macho ya wanadamu, ametuita tujizoeze mambo ya kianalojia ambayo yanaonesha uhusiano wetu na Yeye. Angalia kazi yetu, kwa mfano. Mambo halisi tunayofanya kwa ajili ya Mungu au kwa wanadamu wenzetu yana sifa ya kianalojia wakati wote. Au fikiria kuhusu utunzaji wetu wa Sabato. Ili kuitakasa siku ya Sabato kunahusisha kunahusisha mambo maalum ya utendaji wa kianalojia kama vile kupumzika au kuabudu. Kupumzika kutoka katika shughuli zetu za kawaida na kufanya chaguzi zinazoakisi utakatifu wa siku ya Sabato kamwe sio tukio la kidigitali; daima ni la kianalojia. Hii ni kweli kwa usoefu wa ibada katika kufanya ushirika na wanadamu halisi kanisani kila asubuhi siku ya Sabato. Ingawa inawezekana kujiunga na ibada ya kidigitali kupitia Mtandao, hatimaye usoefu kamili wa ibada hutimilika katika ahadi za papo kwa papo na kushiriki na watu halisi katika maeneo halisi. Matendo ya vitendo na halisi ya wema, neema, msamaha, huruma, hofu, na kuabudu yana maana pale tu tunapohusika moja kwa moja kianalojia.

Hakuna uhalisia wa kimtandao unaoweza kuchukua nafasi au kuzidi mguso halisi wa binadamu kianalojia, busu, mkono wa msaada, faraja ya kukumbatia kutoka moyoni, furaha ya kicheko kinachohisiwa kimwili, au uthabiti wa kupeana mkono kwa ukaribishaji. Hauwezi kusherehekeea kitendo cha kuoshana miguu, au kula mkate na kunywa divai ya meza ya Bwana kwa mtandao. Kile ambacho Yesu alikianzisha kwa njia ya mfano Wake Mwenyewe kinapaswa kukumbukwa kiuhalisia kabisa kwa namna ambayo tunaweza kugusa na kupata muonjo.

Imani Inayoshikika

Hata kitendo cha kufunga na kuomba, kinachositisizwa pote katika Maandiko, ni kitendo cha kianalojia katika wakati na mahali halisi. Imani yetu kwa Mungu daima ina mwelekeo wa analogia ambayo inakuwa ya kuonekana wazi. Ingawa sisi wanadamu tunaweza kufanya kila aina ya mambo kimtandao, uhusiano wetu na Mungu na mwonekano wa kutembea kwetu kiroho na Yesu kamwe hauwezi kupunguzwa kuwa ukweli kimtandao.

Fikiria baraka zote ambazo zinazopatikana katika maisha halisi, zinadhhihirishwa kwa matendo ya kianalojia. "Neno linenwalo wakati wa kufaa, Ni kama machungwa katika vyano vya fedha" (Mithali 25:11). Mkono wa msaada katika kuunga mkono hitaji linaloonekana; mguso wa upole unaoashiria kuwa "Hauko peke yako!"; thamani ya postikadi iliyoandikwa kwa mkono au barua ambayo unashikilia mikononi mwako; upanuzi wa msamaha usiostahiliwa na neema ambayo husababisha uhusiano binafsi uliobadilishwa; kugawana chakula na wale walio na njaa; uzoefu wa ukarimu kwa wale wanaosafiri au kwa wasio na mahali pa kukaa. Haya pamoja na baraka nyingine nyingi zinapaswa kutufikia kianalojia. Furahia mafanikio yako katika ulimwengu wa kidigitali – lakini kumbuka kuwa kianalojia zaidi katika imani yako.

Hebu tuombe pamoja.

Wakati wa Maombi (30 – 45)

Kuomba Kulingana na Neno la Mungu – Ebr. 10:24, 25

“Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia.”

“Tukahimizane Katika Upendo na Kazi Nzuri”

Mungu wetu, tunashukuru kwa kutufunulia ulivyo upendo wa kweli. Tunakushukuru kwa kuutwaa ubinadamu na kutuonesha kupitia Bwana Yesu upendo mkuu. Tunakushukuru, kwa kuwa ulishuka katika ulimwengu wetu na kuishi maisha halisi kianalojia pamoja nasi na kwa ajili yetu. Katika siku na zama hizi za kidigitali, tunaomba utukumbushe uhitaji kamili wa kujihusisha katika ulimwengu wa analogia kwa matendo ya upendo na wema. Mungu wetu, mara nyingi tumekuwa waraibu wa vifaa vyetu na ulimwengu wa mtandaoni. Tunaomba katika jina la Yesu, utukomboe, ili tuweze kuishi kwa ajili Yako kwa kuwatumikia wengine. Amina.

“Wala Tusiache Kukusanyika Pamoja”

Baba, janga la UVIKO-19 liliongeza kasi ya kutenganishwa ambakyo ulimwengu wa kidigitali ulikuwa tayari umekuwa ukituongoza kwa miaka katika utengano. Udanganyifu wa muunganisho wa kweli kupitia njia ya mtandao hautaweza kamwe kuchukua nafasi ya umuhimu na baraka ya mwingiliano halisi wa ana kwa ana. Kwa kuwa sasa janga hili limekwisha tusaidie kutoa kipaumbele katika muunganiko wa moja kwa moja wa wanadamu, tukionesha wema, upendo, kujali, na kutoa msaada kupitia vitendo vinavyoonekana, maneno, na mguso halisi. Tunaomba haya katika jina la Yesu; Amina.

10 SIKU ZA MAOMBI

Mapendekezo Zaidi ya Maombi

Shukrani na Sifa: Shukuruni kwa baraka mahususi na Mumsifu Mungu kwa wema Wake.

Kuungama: Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

Uongozi: Muombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

Kanisa Letu: Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

Mahitaji ya Eneo Mahalia: Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

Sikiliza na Uitike: Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

Mapendekezo ya Nyimbo

- Ni Heri Kifungo. No. 47, 192 (VV).
- Raha Yangu Yote Bwana. No. 190.
- Cha Kutumaini Sina. No. 69, 325 (VV).